Jumapili Novemba 19, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581499

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US



**MBAPPE AZUNGUMZIA BALLON D'OR YA MESSI**

UKURASA 21

UKURASA 3

**Waliopata** ujauzito wafanya mitihani kidato cha nne



UKURASA 3

**Rais** atunuku kamisheni maofisa JWTZ



UKURASA 17

**Weah** akubali kushindwa Uchaguzi




# Matapeli wa mtandaoni wabadili gia angani

• **Mawakala** wabainisha wanavyolizwa, makamanda polisi wakiri ugumu ... *Uk. 4*

# Vivutio uwekezaji Zanzibar vyamkuna Rais wa Romania

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akizungumza na Rais wa Romania, Klaus Lohannis, alipotembelea Ikulu Zanzibar jana. **PICHA : IKULU**

# Mvua yakwamisha ndoa kufungwa

UK. 2

**MICHEZO** **SIMBA YASAKA MAKALI BILA KOCHA MKUU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Vivutio Zanzibar vyamkuna Rais Romania

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Romania, Klaus Iohannis, amesema Zanzibar ni sehemu nzuri kwa uwekezaji na nchi yake itaendeleza ushirikiano katika kuwekeza visiwani humo.

Amesema licha ya uzuri wa uwekezaji, amevutiwa na utamaduni na ukarimu wa wananchi wa visiwa hivyo.

Akizungumza na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi Ikulu Zanzibar, baada ya kuwasili jana visiwani humo, alisema kuna uwezekano mkubwa wa kuendeleza ushirikiano katika sekta ya utalii.

Rais Iohannis alisema ni muhimu Romania na Zanzibar kubadilishana uyamaduni kwa kuzingatia ulinzi na usimamizi wa urithi wa kiutamaduni ili kukuza uchumi.

Kiongozi huyo alieleza kufurahishwa na dira ya maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050 na mwelekeo wake wa mawazo mazuri kuhusu siku zijazo kwa maendeleo ya nchi hiyo.

Rais Mwinyi aliiomba serikali ya Romania kuwekeza Zanzibar katika sekta za uchumi wa bluu, utalii na sekta zingine ili nchi iendelee kupiga hatua za kimaendeleo.

Alisema ukuaji wa nchi na ustawi wa baadaye unategemea uwekezaji na biashara katika uchumi wa bluu na utalii.

Dk. Mwinyi alisema ujio wa Rais huyo umewapa fursa ya kutafakari kuhusu uhusiano na mikakati ya ushirikiano zaidi kwa nchi hizo ili kuendelea kupiga hatua za kimaendeleo.

Rais Mwinyi alipongeza utayari wa kufanya kazi na Zanzibar katika ukuaji wa ustawi huo na hatua kubwa iliyofikiwa na nchi hizo mbili kutokana na historia kubwa ya kidemokrasia iliyowekwa.

Dk. Mwinyi alimthibitishia Rais wa Romania kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kufanya kazi na watu wa nchi hiyo kwa faida ya pande zote mbili.

Alipongeza ujio huo kukaa kwa furaha na kutembelea maeneo ya kihistoria ikiwamo Mji Mkongwe ili kuona mandhari ya Zanzibar na vivutio vya kitalii vilivyokuwapo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Jamal Kassim Ali, alisema ujio wa Rais huyo Zanzibar ni fursa ya kupata wawekezaji kutoka nchini Romania kwenda kuwekeza Zanzibar.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AMINI MOHAMED AMIN**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA ECHO yenye usajili namba: T 870 CRF, CHASSIS NAMBA: JTDKW123603016299 na ENGINE NAMBA: 1JT20FE307. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/6100/2023**



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maluum, Dk. Dorothy Gwajima (katikati), akimkabidhi tuzo Balozi, Getrude Mongella (kulia), iliyotolewa na Tapo la Umajumui wa Wanawake wa Kiafrika (PAWO),ikiwa ni kutambua mchango wake katika kukuza ajenda ya mwanamke na ukombozi nchini, jana, jijini Dar es Salaam. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Mvua yakwamisha ndoa kufungwa

**Na Steven William,** MUHEZA

MVUA inayoendelea kunyesha mkoani Tanga, imesababisha ndoa mbili zilizopangwa kufungwa wikiendi hii, kushindwa kufanyika.

Hiyo imetokana na mabwana harusi wawili waliokuwa wakitoka Segera na Tanga mjini kwenda kuoa katika Tarafa ya Amani wilayani Muheza, kushindwa kuendelea na safari baada ya daraja la Mto Msangazi kufurika maji.

Hali hiyo ilisababishwa na mvua kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia juzi na kufanya zaidi ya abiria 200 ambao walikuwa wakitumia usafiri wa mabasi, malori na pikipiki kukwama eneo hilo.

Mwandishi wa Habari hii alifika eneo la tukio na kukuta abiria waliokuwa kwenye vyombo hivyo vya usafiri wakiwa wamekwama.

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Muheza, Hadija Sokolo, alifika eneo la tukio na kushuhudia hali hiyo huku akiwaonya vijana wenye tabia ya kuvusha watu kwani ni hatari. Mmoja wa maderava hao wa usafiri wa pikipiki, maarufu kama bodaboda, alikamatwa kwa madai ya kukaidi amri.

Kutokana na kuwapo kwa tatizo hilo, Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, alitoa tahadhari kwa wananchi kuwa waangalifu kipindi hiki cha mvua kubwa zilizochangia mito kujaa.

Daraja hilo limekuwa likijaa maji na kusababisha athari kubwa kwa watumiaji ambao hutoka Muheza mjini na maeneo mengine kwenda Tarafa ya Amani.

Mvua zinazoendelea wilayani hapa zimesababisha pia nyumba kadhaa kuzingirwa na maji baada ya kutokea mafuriko katika Mto Amtico, Mtaa wa Genge Kwamtiga juzi na jana.

Aidha, mvua hizo zimesababisha mawasiliano kukatika kwa wakazi wa Soko la Majani Mapana kwenda Kituo cha Polisi cha Mang'enya.

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA AT ARUSHA**

**EXECUTION/CASE NO. 12 OF 2023**

**GIPSON EMERALD OSIMA...........APPELLANT/PLAINTIFF**

**VERSUS**

**BENEZETH MICHAEL & 2 OTHERS...........DEFENDANT/RESPONDENT**

**NOTICE OF HEARING/MENTION**

**TO: BENEZETH MICHAEL MAGANJA**
**P.O. Box 14183, ARUSHA**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention/hearing in the high court at Arusha on the 30 day of November, 2023 at 12:00 o'clock in the forenoon, before **Hon. J.J. KAMALA, DR.**
You may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all documents upon which you intend to rely in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of you appearance on that day and time before mention or hearing the court may proceed in your absence.
A copy of the bill of costs/chamber summons/affidavit/petition of appeal/judgment and decree is attached here to.
**GIVEN under my HAND** and the **SEAL** of the **COURT** this 26 day of OCTOBER, 2023.

DEPUTY REGISTRAR ARUSHA

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA AT ARUSHA**

**EXECUTION/CASE NO. 12 OF 2023**

**GIPSON EMERALD OSIMA...........APPELLANT/PLAINTIFF**

**VERSUS**

**BENEZETH MICHAEL & 2 OTHERS...........DEFENDANT/RESPONDENT**


**NOTICE OF HEARING/MENTION**

**TO: PREMIUM REAL ESTATE & PROPERTIES LTD**
**P.O. Box 14183, ARUSHA**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention/hearing in the high court at Arusha on the 30 day of November, 2023 at 12:00 o'clock in the forenoon, before **Hon. J.J. KAMALA, DR.**
You may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all documents upon which you intend to rely in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of you appearance on that day and time before mention or hearing the court may proceed in your absence.
A copy of the bill of costs/chamber summons/affidavit/petition of appeal/judgment and decree is attached here to.
**GIVEN under my HAND** and the **SEAL** of the **COURT** this 26 day of OCTOBER, 2023.

DEPUTY REGISTRAR ARUSHA

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**NATHANIEL NALOGWA MALUILA** naomba kutangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria namba TAE014624 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji makao makuu tarehe 12/03/2018. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBE/KYE/RB/254799/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**RAMADANI SALIMU MNDEME**

anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki aina ya SKY GO zenye usajili namba **T 186 BSP** na **T 135 BYN**, CHASSIS NAMBA: **LF3PCJ706BB001955** na **LF3PCJ700CB000916** na ENGINE NAMBA: **156FMI2B5039248** na **156FMI2C5028004**. Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/6758/20233.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WATOTO YA DAR ES SALAAM**
**KISUTU**
**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI/KINAI NO. 424 YA MWAKA 2023**
**ROBI SIMON MAGAIGWA.........MDAI**
**DHIDI YA**
**ATHUMANI YUSUFU KIONE.........MDAIWA**
**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mdai ameleta maombi yake ambayo maelezo ya Mdai Yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo yanaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo inakuhitaji kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 21/11/2023 saa 2:00 Asubuhi

**ANGALIA:**

Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, utaweza kusikiliza maombi hayo na kutoa hukumu.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 2 Mwezi 11, 2023

HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI MAHAKAMA YA WATOTO KISUTU DAR ES SALAAM

HABARI KITAIFA

# Waliopata ujauzito, kujifungua wafanya mitihani kidato cha nne

**Beatrice Shayo**

WANAFUNZI wawili wa kidato cha nne ambao walikatisha masomo kwa ujauzito, baada ya kujifungua, wanaendelea kufanya mitihani ya kitaifa.

Kati yao yuko ambaye alibakwa akiwa njiani akienda nyumbani ambaye mtoto wake jana amefikisha umri wa siku tisa jijini Dar es Salaam. Kuendelea huko na masomo kwa wasichana hao ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan

Hayo yalibainishwa jana na Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Jokate Mweglo, alipotembelea wanafunzi hao ambao walipata ujauzito na kuendelea na masomo na sasa wanaendelea kufanya mitahani ya kidato cha nne.

Mwegelo alisema amefurahishwa na ujasiri wao wa kuchangamkia fursa ya Rais Samia ya kuruhusu waliopata ujauzito kuendelea na mafunzo. "Nimefika katika familia hizi mbili Mbagala Kisewe na Chamanzi ikiwa ni sehemu ya majukumu yangu UWT na kuzungumza na wanafunzi kujua changamoto zao. Niliposikia kuna hao wanafunzi walikuwa wajawazito wamejifungua na wanaendelea na mitihani, nikasema nije kuwaona hao mabinti jasiri waliochangamkia fursa ya Rais Samilia ili wafikie ndoto zao," alisema.

Mwegelo alisema uamuzi wa Rais Samia aliyoyafanya ya wanafunzi kupata ujauzito na kuendelea na masomo ni jambo sahihi la kuwakomboa vijana hususani watoto wa kike kufikia ndoto zao.

Pia alisema watoto wengi unakuta wanaingia kwenye changamoto sio kwamba wametaka ila kuna mambo mbalimbali yanaweza kuchangia ikiwemo kurubuniwa, kukosa malezi sahihi kwa wazazi na changamoto za kiuchumi.

"Ndio maana nimesisitiza sisi kama wazazi tujue nafasi zetu. Wazazi wa kike na kiume, migogoro ndani ya nyumba isiwe sababu ya watoto kushindwa kupata upendo na malezi kwani huo ndio msingi wa kuwajenga watoto wao kwenye kesho yao kwa kuzingatia wanakuwa na maadili mema," alisema Mwegelo.

Alisema changamoto kubwa katika familia hizo mbili amebaini ni migogoro na maisha magumu yaliyosababishia watoto hao kuingia katika mazingira magumu, hivyo wazazi wa pande mbili ni jukumu lao kuwalea watoto wao. Mwegelo alisema atakutana Wizara nne ambazo ni Wizara za Afya; Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Fedha ambazo moja kwa moja zinagusa maslahi ya wananchi.

Alisema serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inaendelea kupunguza vikwazo vya wazazi kushindwa kuwapeleka watoto shule na ndio maana imeanzisha utaratibu wa elimu bila malipo na bado wana nafasi ya kufanya zaidi husussani ya kuwezesha jamii kiuchumi ili wananchi wanufaike.

Asha Khalifan, ambaye ni mzazi wa mwanafunzi mwenye mtoto wa miezi miwili, alisema amejikuta anawalea watoto wake katika mazingira magumu kutoka na kutekelezwa na mume wake baada ya kujikuta anajifungua watoto kike.

Alisema hali hiyo imechangia kushindwa kuwafuatilia watoto wake kwa umakini kwani hata nyumba anayoishia ambayo haina mabati amefadhiliwa na msamaria mwema.

Mzazi wa mwanafunzi wa pili ambaye anaishi Mbande Kisewe, alisema mtoto wake alibakwa akiwa anatoka shule na mpaka sasa wahusika hawajapatikana.

Alisema kuna wakati aliondoka na kumuacha binti yake akiwa amejipangia chumba katika kipindi cha mwaka mmoja huku akiwa anatafuta maisha kwani alikuwa kwenye wakati mgumu baada ya mume wake kumkimbia wakiwa wanadaiwa kodi ya nyumba.

Alisema baada ya baba yao kuwakimbia, walifukuzwa katika nyumba na mwanafunzi huyo kuishi maisha yankujitegemea bila mzazi yoyote kumfuatilia.



Rais, Samia Suluhu Hassan, akikagua gwaride wakati alipo tunuku Kamisheni kwa Maofisa wanafunzi Kundi la 04/20-shahada ya Sayansi ya Kijeshi na Kundi la 70/22 (Regular) Monduli Mkoani Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# EWURA yaanika kikwazo gesi magari

**Na Vitus Audax**, MWANZA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imesema kwa sasa mikoa ya Kanda ya Ziwa kupata huduma ya Nishati ya Gesi asilia kwa ajili ya magari (CNG) si jambo rahisi kutokana na umbali uliopo na maeneo inapozalishwa nishati hiyo.

Mfumo huo unaoelezwa kupunguza gharama kwa asilimia 40 kulinganisha matumizi ya petroli na dizeli ambazo zimekuwa zikiendelea kupanda kila uchao, umekuwa kimbilio la wamiliki wa magari wengi mkoani Dar es Salaam ambako tayari wawekezaji mbalimbali wamejitosa kutoa huduma hiyo.

Akizungumza na Nipashe juzi, Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, Mhandisi George Mhina, alisema suala la upatikanaji wa nishati hiyo kwa magari katika mikoa ya Kanda ya Ziwa hususani Mwanza bado ni gumu.

Hali hiyo alisema inatokana na asili yake kuhitaji kusafirishwa kwa njia ya mabomba ambayo bado hayajafika.

Pia alisema endapo itasafirishwa kwa njia ya magari umbali usizidi kilomita 500, itasababisha gharama kuwa juu na kuondoa maana ya kutumia mfumo unaotajwa kuwa nafuu zaidi.

"Ni sahihi kuwa kwa sasa kuna uhitaji mkubwa wa mfumo huu. Mikoa yetu hususani kwa jiji kama Mwanza ambapo tumekuwa tukiona unaendelea kutumiwa na watu wengi katika mikoa Dar es Salaam kutokana na ukaribu wake na eneo la uzalishaji,"alisema Mhandisi Mhina

Mhandisi Mhina alisema lengo kubwa la kutumia mfumo wa gesi asilia kwa magari ni kurahisisha gharama kutokana na mfumko wa bei kwa mafuta pamoja na kudhibiti uchafuzi wa mazingira hivyo kusafirishwa umbali mrefu pia kunaweza kuongeza gharama za huduma hiyo kinyume cha uhitaji.

"Kwanza asili ya gesi ikisafirishwa umbali mrefu inaharibika na kupunguza ubora wake wa awali, hivyo kwa mikoa yetu ya mbali inaweza ikachua muda mrefu labda serikali iwekeza kwenye mtandao wa mabomba ya kusafirisha nishati hiyo kwa mikoa yetu,"alisema.

## Rais atunuku kamisheni maofisa wapya wa JWTZ

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewatunuku kamisheni maofisa wanafunzi 575 wa kundi la nne la mwaka 2020, Shahada ya Sayansi ya Kijeshi (BMS) pamoja na kundi la 70 la kawaida la mwaka 2022 cheo cha Luteni Usu.

Maofisa hao waliotunukiwa kamisheni na Rais Samia jana katika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi (TMA) Monduli. Kati yao wanaume ni 482 na wanawake ni 93.

Baada ya Rais Samia kutunuku kamisheni alitoa zawadi kwa maofisa wanafunzi waliofanya vizuri zaidi kwa makundi yote mawili na kumvisha bawa ofisa mwanafunzi, Rubani Amour Mohamed kwa niaba ya marubani wenzake.

"Naamini mafunzo haya yatawaongezea weledi wanafunzi wote na hongereni sana wote," alisema Rais Samia.

Katika kundi la nne la mwaka 2020 la shahada ya sayansi ya kijeshi, mshindi wa jumla kwa fani zote ni ofisa mwanafunzi Mihinzo Jafari, Maria Jafari (mshindi katika taaluma), Saria Mkwele (medani) na mshindi wa jumla wa kundi la wanawake ni Grace Ng'ondya.

Pia katika kundi la 70 la mwaka 2022 wa kawaida (regular) mshindi wa jumla ni ofisa mwanafunzi Fickson Ngenje huku Shabani Adam Shaban akiibuka mshindi wa taaluma Shukuru Saria (medani) na mshindi wa jumla kwa wanawake ni Nuru Ngabo.

Mkuu wa Chuo Cha Mafunzo ya Kijeshi TMA, Bregedia Jenerali Jackson Mwaseba, alisema maofisa wanafunzi hao wamekuwa maofisa wa Jeshi la Ulinzi la Wanachi wa Tanzania (JWTZ) na maafisa wapya wa kundi la nne la mwaka 2020 62 wamepata mafunzo katika chuo cha TMA kwa muda wa miaka mitatu na kuhitimu shahada ya sayansi ya kijeshi.

Pia alisema kundi la 70 la mwaka 2022 (regular) lenye maofisa 447 wamepata mafunzo hayo kwa muda wa mwaka mmoja miongoni mwao maofisa 66 wamepata mafunzo nje ya nchi marafiki.

"Miongoni mwao wako maafisa wanafunzi Watanzania 66 waliopata mafunzo yao kutoka nchi rafiki Afrika Kusini (watatu),Bangladeshi (mmoja), China (tisa), Kenya (wanane), Malawi (mmoja),Misri (sita), Sri Lanka (wawili ) na Russia 30," alisema.

Alisema wanafunzi 88 wa makundi yote mawili wameachishwa mafunzo kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo kukosa utimamu wa mwili, tabia isiyoridhisha, kutofikia viwango kitaaluma, kukosa uaminifu na ugonjwa.

Jenerali Mwaseba alisema chuo kinaona fahari kubwa kwani hiyo ni mara ya kwanza kuwezesha mafunzo ya shahada hiyo kwa kujisimamia pasipo na ushirikiano wa kimafunzo na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA).

Sherehe hizo zimehudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, Mkuu wa Majeshi, Jenerali Jacob Mkunda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Faraji Mnyepe na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Yussu Masauni.

## HABARI KITAIFA

# Matapeli mtandaoni walivyobadili gia angani

**Na Waandishi Wetu**

"TAFADHALI tuma pesa kwa namba hii." Huu ni ujumbe mfupi wa maandishi ambao umekuwa ukiwafikia wateja wengi wa simu za mkononi kutoka kwa matapeli huku wengine wakipigiwa simu kuwa watoto wao walioko shule za bweni wanaumwa hivyo watume fedha za matibabu.

Utapeli huu wa mtandaoni umeshika kasi nchini huku wananchi kutoka mikoa mbalimbali wakifunguka namna walivyolizwa kwa kuibiwa fedha zao na mbinu za matapeli hao zikibadilika mara kwa mara.

Mbinu wanazotumia ni baadhi kujitambulisha kama watumishi katika kampuni za simu au watu wa karibu wa wanaowatapeli, wengine hujifanya kuwa na wagonjwa mahututi na walio wengi wakilizwa kupitia ujumbe usemao, 'Ile hela nitumie kwa namba hii'.



Janeth Magomi

### WAATHIRIKA WASIMULIA

Msaidizi wa ndani aliyejitambulisha kwa jina la Mwamini (la pili linahifadhiwa) mkazi wa Dar es Salaam, alisema Novemba 6, mwaka huu, akiwa nyumbani kwa bosi wake asubuhi, alipokea ujumbe wa fedha wa Sh. 580,000 katika simu yake.

"Nilipopata huu ujumbe nikaona nimepata mtaji huwezi amini nilimfuata bosi wangu nikamwambia ninaomba kuacha kazi, naye akashangaa mbona ghafla. Nikamdanganya ninahitajika nyumbani na tayari nilikuwa nimeshawapanga wazazi endapo angewapigia," alisema.

Baada ya dakika kadhaa, anasema alipigiwa simu kutoka kwa mwanamume akijitambulisha kama mfanyakazi wa kampuni ya simu (jina linahifadhiwa) akimtaka azirejeshe fedha alizopokea.

Alisema mtu huyo alimwambia kuwa fedha zilikuwa zinatumwa kwa mtu mwingine hospitalini Temeke mwenye mgonjwa aliyeko chumba cha wagonjwa walio katika uangalizi maalum (ICU), lakini wakala akakosea namba.

"Akanitaka niende kwa wakala haraka kutuma na alinipa masharti nisimwambie mtu yeyote hata wakala nisimwonyeshe huu ujumbe wa fedha zaidi nikifika nimwambie atume hizo fedha. Wakati wote huo nilikuwa sijaangalia salio.

"Nikaenda kwa wakala ingawa aligoma kutuma akataka fedha taslimu wakati sikuwa nazo. Huyu tapeli alikuwa ananipigia simu kila mara. Nilipomwambia wakala amekataa, akaniambia nikachukue zangu, kweli nikarudi nyumbani.

"Kutokana na simu zake kuwa nyingi njiani, niliamua kumshirikisha bosi wangu, ndipo aliponifungua kuwa huyo ni tapeli, akaniambia niangalie salio langu, nilikuta Sh. 234.25 tu. Bosi wangu alipoongea na huyo mtu, aliambulia matusi ya nguoni, ndiyo ikawa salama yangu," alisema.

Mkazi wa Kilimanjaro ambaye hakutaka jina lake litajwe, alisema alipokea simu ya mtu aliyejitambulisha kama mpangaji wa zamani nyumbani kwao akiomba msaada wa mtu wa bodaboda ampelekee chakula.

"Nilimtafuta mtu wa bodaboda ninayemfahamu ambaye pia anamjua huyo mpangaji wa zamani nyumbani kwetu. Nikampa simu wakaongea naye akamwelekeza alipo, nikarudi nyumbani kuendelea na shughuli zangu.

"Baada ya muda kidogo nikapigiwa simu na bodaboda kuwa yule hakuwa mpangaji bali ni tapeli ambaye njiani aliendelea kuwasiliana naye akampa maelekezo mengine.

"Akamtaka bodaboda atafute wakala anayemwamini ili amtumie Sh. 200,000 alafu akishampelekea chakula atampa taslimu ili ampitishie wakala naye akafanya hivyo na alipofika eneo alilotakiwa kupeleka chakula, alipoipiga ile namba ikawa haipatikani.

"Alipokwenda kazini kwa mpangaji, mpangaji alishangaa kwa kuwa siku hiyo alikuwa hajafanya mawasiliano na mtu yeyote," alisimulia huku akisema kitendo hicho kimesababisha aingie katika madeni ya kulipa fedha hizo baada ya suala hilo kufikishwa polisi.

Mkazi wa Mtaa wa Chuda jijini Tanga, Fatma Mfaume, alisema: "Nilipigiwa simu kuambiwa mtoto wangu anaumwa shuleni. Bila kujifikiria mara mbili, nikajikuta nimetuma fedha."

Mkazi wa Daraja Mbili, jijini Arusha, Ezekiel Kivuyo, anasimulia alivyotapeliwa Sh. 200,000 baada ya kupokea simu ya mtu akijitambulisha kama mwimbaji wa nyimbo za injili (jina linahifadhiwa).

John Kasikia, mkazi wa Ginnery Manispaa ya Singida, alisema alitapeliwa Sh. 600,000 baada ya kupigiwa simu na mtu akijitambulisha kwa jina sahihi la mkuu wa shule ambayo mtoto wake anasoma Shule ya Sekondari Mbeya pamoja na namba.

Mkazi wa Kahama, Colletha Kapongwa, anasimulia alivyotapeliwa Sh. 500,000 baada ya kupokea simu ya mtu akimtaja kwa majina yake kamili akidai anafanya biashara za kusafirisha mizigo, hivyo amekwama nauli Sh. 900,000 na alipotuma mtu huyo alizima simu.




Jabir Bakari.

Sophia Josia, mkazi wa Dodoma mjini, alisema utapeli huo umeongezeka kwa watu kuambiwa kuna kiasi cha fedha kimeingia katika simu na kutakiwa kukirejesha wakati si kweli.

### MAWAKALA WALIZWA

Wakala anayetoa huduma katika Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, Loyce Bernard, anasimulia alivyotapeliwa Sh. 700,000 baada ya matapeli kumtumia ujumbe ukionyesha umetoka kwenye namba ya bosi wake.

Wakala Yukunda Anthony mkazi wa Moshi, Kilimanjaro, alisema kwa Oktoba pekee yake, amenusurika kutapeliwa kwa mbinu mbalimbali zaidi ya mara 23 na ameokoa wateja waliotaka kuwatumia fedha matapeli 16.

Tatu Jumanne, ambaye ni wakala katika Kituo Kikuu cha Mabasi yaendayo mikoani cha Moshi, alisema alitapeliwa Sh. 700,000 na kwamba licha ya kutoa taarifa Kituo Kikuu cha Polisi Moshi Mjini, hadi sasa ni mwaka na hakuna kilichofanyika zaidi ya kupigwa kalenda na mpelelezi aliyekabidhiwa.

### MAKAMANDA WAFUNGUKA

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Blasius Chatanda, alikiri kuwapo kwa matukio hayo mkoani mwake na mengine yakihusisha laini zaidi ya moja, hivyo polisi huhitaji muda kuwabaini wahalifu hao.

"Hawa matapeli ni wengi na wana majina tofauti unaweza kushughulika na jina la Mussa kumbe ni Isaya na yuko hata mkoa mwingine. Tunachokifanya ni kufanya mawasiliano na kampuni ya simu kwanza ndipo tunaanza kufuatilia," alisema Kamanda Chatanda.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martine Otieno, aliahidi kutoa takwimu za mkoa kesho huku akibainisha kuwa wanaotapeliwa, wengi ni wanaoishi vijijini huku akitaka elimu iendelee kutolewa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Mchunguzi, alikiri kuwapo kwa kesi nyingi za wizi wa mitandaoni mkoani humo na wako waliokamatwa na kufikishwa mahakamani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema: "Tunacho kitengo cha ufuatiliaji kimtandao, hivyo tukipokea taarifa tunafuatilia."

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, alisema, "Andika barua ya kuomba hizo takwimu, ili na sisi tuanze kuzitafuta, lakini hatuna kwa sasa," alisema Kamanda Maigwa.

### TCRA YATAJA NAMBA

Meneja wa Mamlaka ya Mawasilino Tanzania (TCRA), Kanda ya Ziwa, Mhandisi Francis Mihayo, alisema kabla ya usajili wa alama za vidole kufanyika walikuwa wakipokea kwa siku simu tano za malalamiko sasa wanakaa muda.

Alisema kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa kudhibiti matukio hayo kwa kutoa elimu kwa jamii huku wakitoa namba ya huduma ya usaidizi 100 ambayo inatumiwa na kampuni za simu au kutuma ujumbe wa utapeli kwa namba 15040 kwa kutuma namba yake.

"Tukipata ujumbe huo namba husika tunazifungia huduma na zinakuwa haziwezi tena kuendelea kufanya utapeli wa aina hiyo. Wananchi waepuke sana vijana wanaosajili laini hovyo mitaani hasa wanaotumia kigezo cha kusajili laini za chuo wakati wewe (unayesajiliwa) unaishi eneo ambalo hakuna chuo.

"Ukiona hivyo piga namba 100 kuwasiliana na kampuni ambayo anataka kukusajilia laini ili kujiridhisha kama wanamtambua?" alisema Mihayo.

Oktoba 25, mwaka huu, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabir Bakari, akiwa jijini Arusha, alitoa takwimu za kufungiwa namba za simu 34,848 zilizoripotiwa kupotea, kuibiwa na kuhusika katika matukio ya uhalifu katika kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka huu.

Pia alisema TCRA imezifungia laini 23,328 za simu zilizobainika kuhusika na viashiria vya ulaghai kuanzia kipindi hicho ikilinganishwa na 23,234 kati ya Aprili hadi Juni mwaka huu.

Dk. Bakari alisema kufungiwa kwa simu hizo, pia kumewezesha kupunguza matukio ya wizi na kusaidia upatikanaji wa vifaa vya mawasiliano vyenye ubora.

## HABARI KITAIFA

# Wanafunzi 3,000 kunufaika elimu uhasibu, fedha

**Na Joseph Mwendapole**

KATIKA jitihada za kuandaa wahitimu wanaoendana na soko la ajira duniani, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), kimeingia kwenye ushirikiano na kampuni ya RSM Eastern Africa kuwajengea uwezo wanafunzi wake katika uhasibu na elimu ya fedha.

Kupitia ushirikiano huo, RSM itatoa mafunzo kwa wanafunzi wa chuo hicho katika maeneo matatu ambayo ni ukaguzi wa hesabu, elimu ya kodi na ushauri wa kitaalamu.

Akifungua mafunzo hayo jana chuoni hapo, Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, anayeshughulikia Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Emmanuel Munishi, alisema mafunzo hayo yatatolewa pia kwa wanafunzi wa vyuo vingine. "CBE itakuwa kituo tu au Hub (kitovu) ya mafunzo hayo kwa taasisi zote za elimu ya juu Tanzania na kwenye program hii, tunatarajia kuwanufaisha wanafunzi 3,000 wanaosomea shahada za uhasibu, uhasibu na fedha, na taaluma ya benki na fedha,"alisema.

Prof. Munisi alisema mafunzo hayo ambayo yataendeshwa na maafisa waandamizi kutoka RSM Eastern Africa wenye uzoefu wa kimataifa yatasaidia ajenda ya maendeleo ya kimataifa.

Pia alisema mafunzo hayo yatasaidia kwenye kufikia lengo la nne la Maendeleo Endelevu la Umoja wa Mataifa kuhusu elimu bora na hasa elimu ya ufundi na elimu ya fedha ambayo inatolewa na chuo cha CBE.

Alisema mafunzo hayo yatahitimishwa na mashindano a washiriki ambapo washindi watapewa nafasi za masomo kwa vitendo yaani internship na yatasaidia jitihada za chuo kuwaandaa wahitimu kwaajili ya soko la ajira.

Prof. Munishi alisema RSM imekuwa ikifanya kaguzi za hesabu za fedha CBE kwa miaka sita iliyopiyta na kwa miaka yote hiyo chuo kimekuwa ikipata hati safi na hoja ambazo wamekuwa wakiziibua CBE imekuwa ikizifanyia kazi. "Mafunzo haya ni muhimu sana kwa wanafunzi wetu wa CBE na yatatolewa na watu waliobobea kwenye masuala ya ukaguzi hivyo naona wanafunzi mtakaoshiriki kwenye program hii mnabahati kubwa sana na yatasaidia ajenda ya maendeleo ya kimataifa," alisema.

Prof. Munishi alisema serikali imefanya maboresho makubwa kwenye mitaala ya elimu na moja ya eneo ambalo imesisitiza ni wanafunzi kusoma kwa vitendo na kwamba elimu ya fedha na biashara ipewe umuhimu wa kipekee.

"Kwa hiyo nyinyi wanafunzi ambao mnasomea uhasibu, fedha, benki na biashara mko katika mazingira mazuri ya kuajiriwa na kujiajiri mtakapomaliza masomo kwa sababu kila kitu duniani kwa sasa kinatoa umuhimu kwa fani hizo," alisema.

Naye Jovin Bhoke, ambaye ni Meneja wa Kodi wa Kampuni ya RSM, alisema kila mwaka huwa wanaadhimisha siku ya huduma kwa wateja kwa kufanya shughuli mbalimbali za kusaidia jamii.

Alisema katika shughuli hizo huwa wanaangalia ajenda za serikali na zile za kidunia ambapo kwa sasa wameangalia ajenda namba nne ya UN inayojihusisha na utoaji wa elimu bora. "Tumechagua kuja CBE kwa sababu ni chuo kikongwe kwenye kutoa elimu ya biashara, kodi na elimu ya fedha na tutawashirikisha kile tunachokifanya ili wanafunzi wawe wanasoma kwa kwa vitendo masuala yanayohusu elimu ya fedha," alisema Bhoke.

Alisema RSM ni taasisi ya kimataifa inayojihusisha na masuala ya ukaguzi wa hesabu za fedha, elimu ya kodi, kutoa ushauri wa kitaalamu wa na uzoefu wa kimataifa wa kufanyakazi katika zaidi ya nchi 120 duniani katika mabara ya Afrika, Asia, Ulaya na Amerika.

# Wajasiriamali vijana wataja mbinu kufanikiwa kimaisha

**Na Restuta James**

WAJASIRIAMALI vijana wanaotekeleza mawazo bunifu wametoa mbinu kwa vijana kufanikiwa katika biashara wakibainisha kuwa uvumilivu na kutobadili maono ni zana muhimu kujenga taasisi za kibunifu.

Vijana hao waliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kwenye mjadala wa Wiki ya Kimataifa ya Ujasiriamali ulioandaliwa na Ubalozi wa Marekani nchini na kuwakutanisha wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tanzania Startup Association (TSA), inayosaidia kampuni changa na mawazo bunifu, Zahoro Muhaji, alisema ujasiriamali unahitaji watu jasiri wenye nia ya kuleta mabadiliko chanya kwa kutatua changamoto zinazoikabili jamii na dunia.

"Ujasiriamali si kwa ajili ya kila mtu na mimi sitamshauri kijana aingie kwa sababu amekosa ajira. Ili uufanye kwa ufanisi, ni lazima uupende, uwe tayari kujihatarisha maana kuna wakati unaweza kupoteza hela yako yote, utavunjika moyo lakini ukiwa na maono ya kile unachofanya utavumilia njia unayopita," alisema.

"Kama unataka kuwa mjasiriamali na hauna ajira, anza biashara ndogo itakayokupa fedha zitakazokupa nguvu ya kutekeleza wazo lako kwa sababu ujasiriamali unahitaji muda kukua," alifafanua.

Mkurugenzi na mwanzilishi wa taasisi ya Accelerate inayotoa ushauri wa kitaalamu kwa wajasiriamali na waajiri, Bernice Fernandes, alisema Tanzania kuna fursa nyingi za kufanikiwa kutokana na kuwapo kwa changamoto nyingi zinazowakabili wananchi.

Hata hivyo, alishauri kuwa vijana wanapopata nafasi ya kuajiriwa wanapaswa kufanyakazi kwa bidii.

"Kufanikiwa kunakuhitaji hata ukiajiriwa ufanye kazi za ziada ili mwenye ofisi akuone kama mtu mwenye nafasi ya kushirikiana naye zaidi. Usiishie tu kufanyakazi yako uliyoajiriwa nayo, fanya za ziada ambazo ziko ofisini kwako, tafuta pia kujua kama unafanyakazi kwa tija, hii itakusaidia kupata mbinu mpya zitakazokufaa kwenye safari yako ya ujasiriamali," alisema.

Bernice aliongeza kuwa: "Mtandao umeongeza nafasi ya kujifunza ubunifu na utendaji, ni vyema kutumia njia hizi kupata ujuzi mpya."

# TANGAZO/ NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD; TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED; MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD na MBUZAX AUCTION MART & COMPANY LIMITED,** kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya Siku Kumi na nne (14) na Siku Saba (7) kama rudio la tangazo kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PETER DANIEL NYIKA | PETER DANIEL NYIKA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK 011077, ARDHI NA.TMK/MBGL/KGG34/217 | KINGUGI, MBAGALA MANISPAA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 04/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 2 | SALUM OMARI AMIRI | SALUM OMARI AMIRI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | MWANDEGE, VIKINDU KATA YA MKURANGA | 04/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 3 | CHESCO K. MWALONGO | CHESCO K. MWALONGO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | ULONGONI, GONGO LA MBOTO, MANISPAA YA ILALA | 06/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 4 | ERICA M. PAULO | ERICA MKUMBI PAULO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | KILUNGULE 'A', KIMARA, MANISPAA YA KINONDONI | 10/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 5 | YUDA THADEUS LYIMO | YUDA THADEUS LYIMO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA. TMK020871, ARDHI NA.TMK/YBV/BMW28/57 | BARABARA YA MWINYI, YOMBO VITUKA, MANISPAA YA TEMEKE | 11/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 6 | YAHAYA YUSUPH KASEKE | YAHAYA YUSUPH KASEKE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK044735, ARDHI NA.TMK/KEK/MWGB9/147 | KEKO, KEKO MWANGA B, MANISPAA YA TEMEKE | 13/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 7 | JACOB MELICHON MWAJOMBE | JACOB MELICHON MWAJOMBE | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MBONDE, KIBAHA, WILAYA YA PWANI. | 15/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 8 | DOTTO PETER MADUKWA | LEYLA KHALIDY AHMED SHEBE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.161600, PLOT NA.209, BLOCK 'A' | MBANDE, MANISPA YA TEMEKE | 18/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 9 | AKIDA RAMADHANI MWAIMU | AKIDA RAMADHANI MWAIMU | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND024459, ARDHI NA.KND/KWE/MGJ15/98 | MAKONGO JUU, KAWE MANISPAA YA KINONDONI | 20/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 10 | MANASA MANDITI | MANASA OMARI MANDITI | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.028511, ARDHI | UKWAMANI, KAWE MANISPAA YA KINONDONI | 21/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 11 | JOYCE GWALUGANO MWASABWITE | GWALUGANO OBASI MWASABWITE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.34098, PLOT NA.304, BLOCK 'G' | MBAGALA, MANISPAA YA TEMEKE | 05/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 12 | CAPEVIEW COMPANY LIMITED | MUSSA SIMBA KALIMANZILA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK042322, ARDHI NA.TMK/MBGK/KJC7/129 | MTONI KIJICHI, MBAGALA KUU, MANISPAA YA TEMEKE | 05/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 13 | PAUL JULIAS WANGUBO | PAUL JULIAS WANGUBO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.ILA029742, ARDHI NA.ILA/KTD/KPNB18/88 | KIPUNGUNI B, KITUNDA, MANISPAA YA ILALA | 08/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 14 | PASTORI CLAUD MODU | PASTORI CLAUD MODU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | SABASABA UKONGA, MANISPAA YA ILALA | 16/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 15 | DONATI ANDREA MATENTELE | EMMANUEL MARTIN SIMBA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.69175, PLOT NA.196, BLOCK NA.1 | MWANAGATI, MANISPAA YA ILALA | 14/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITE |
| 16 | DONATI ANDREA MATENTELE | DONATI ANDREA MATENTELE | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | MBONDOLE, MSONGOLA MANISPAA YA ILALA | 14/12/2023, SAA 08:00 MCHANA NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 17 | VINCENT SELINA MATONYA | VINCENT SELINA MATONYA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.ILA018278, ARDHI NA.ILA/UKG/MDF14/37, | MWEMBE MADAFU, KONGA, MANISPAA YA ILALA | 22/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 18 | SIMON YASINTO MILANZI | SIMON YASINTO MILANZI | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK002779, ARDHI NA.TMK/MBGK/MTT8/39A, | MWANAMTOTI, MBAGALA KUU, MANISPAA YA TEMEKE | 21/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 19 | ABDALLAH HASSANI JUMA | ABDALLAH HASSANI JUMA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK045156, ARDHI NA.TMK/CHB/RTT35/300A | RANGI TATU, CHARAMBE MANISPAA YA TEMEKE | 23/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 20 | ABDALLAH HASSANI JUMA | ABDALLAH HASSANI JUMA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK045157, ARDHI NA.TMK/CHB/RTT35/300 | RANGI TATU, CHARAMBE MANISPAA YA TEMEKE | 23/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 21 | JAMILA MOHAMED YAHAYA | JAMILA MOHAMED YAHAYA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK015576, ARDHI NA.TMK/MKW/BUZ8/38 | BUZA, MAKANGARAWE MANISPAA YA TEMEKE | 20/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 22 | HUSNA RAMADHANI MAULID | DELVIS J. WASEDA, HUSNA MAULID & MIRAN WASEDA | KIWANJA CHENYE HATI YA MAUZIANO | MGEULE JUU, BUYUNI MANISPAA YA ILALA | 06/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MBUZAX AUCTION MART & COMPANY LIMITED |
| 23 | PATRICIA ANURUPHUS MPANJU | ANURUPHUS MPANJU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | MADALE, WAZO MANISPAA YA KINONDONI | 27/11/2023 , SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD | MBUZAX AUCTION MART & COMPANY LIMITED |
|---|---|---|---|
| P.O.Box 68172 | P.O.BOX 1305 | P.O.Box 12943 | P. O. Box 62070 |
| Dar es Salaam, Tanzania | Songea, Ruvuma | Arusha, Tanzania | Dar es Salaam |
| Tel: 0620 848 565/ 0714 598 559 | Tel: 0757 940 064/ 0716 070 298 / 0784 718 734 | Tel: 0752 632 033/ 0628512033 | Tel: 0755506970, 0716763571 |
| Email: lehalelglc@gmail.com | Email: twinscoltd5@gmail.com | Email: mangwembe@gmail.com | |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maoni ya wadau miswada sheria yazingatiwe na kufanyiwa kazi

**SERIKALI** katika Mkutano wa 13 wa Bunge uliomalizika wiki iliyopita, iliwasilisha miswada ya sheria ya uchaguzi, vyama vya siasa na tume ya uchaguzi ambayo ilisomwa kwa mara ya kwanza. Miswada hiyo inatarajiwa kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye kujadiliwa na kupitishwa kabla ya kutiwa saini na Rais kuwa sheria.

Kutokana na kuwasilishwa huko, serikali imetoa rai kwa wadau, kama ilivyo ada, kutoa maoni yao yatakayowezesha kuboreshwa kwa miswada hiyo. Aidha, kwa kufanya hivyo, wananchi watakuwa wameshirikishwa kueleza wanayoona yanafaa kwa manufaa na maslahi mapana ya taifa. Wananchi wamepewa miezi mitatu kutoa maoni yao kabla ya Mkutano wa 14 wa Bunge utakaofanyika Februari, mwakani miswada hiyo itakapojadiliwa na kupitishwa.

Kwa ujumla, miswada hiyo ina lengo la kuwapo kwa tume huru ya uchaguzi ambayo itakuwa na wajumbe watakaopatikana kwa njia ya usaili badala ya mfumo uliopo ambao unatoa mamlaka kwa Rais kuwateua jambo ambalo lilikuwa linalalamikiwa na baadhi ya wadau wa siasa kwamba linaifanya isiwe huru. Kwa maneno mengine tume ya sasa ilibatizwa jina la Tume ya CCM na inaamua kwa kufuata maelekezo ya chama tawala na walioko madarakani.

Katika msingi wa hoja zao, wadau wengi wanaegemea katika uchaguzi mkuu uliopita wa mwaka 2020 na ule wa serikali za mitaa wa mwaka 2019 kuwa haukuwa huru na wa haki kutokana na hali iliyokuwa huku baadhi ya wasimamizi wakitishiwa na mamlaka za juu za serikali kwamba iwapo wapinzani watashinda, watambue kwamba hawana kazi.

Kwa desturi na kwa muda mrefu, wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa wamekuwa wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo, hivyo kwa mujibu wa wadau, kuwapo kwao na kuendelea na jukumu hilo, kunatoa nafasi ya upendeleo kwa chama tawala kwa kuwa wao ni watumishi wa serikali iliyoko madarakani na hawana uhuru kamili wa kutoa uamuzi.

Wiki hii, kulikuwa na mjadala wa kitaifa kuhusu miswada hiyo na watu mbalimbali, wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa, walitoa madukuduku yao huku baadhi wakipongeza hatua anazozichukua Rais Samia Suluhu Hassan za kuimarishwa kwa demokrasia na utawala bora tangu alipoingia madarakani mwaka 2021.

Mbali na viongozi wa vyama vya siasa, wengine waliojitokeza ni asasi za kiraia (AZAKI) na taasisi za sheria na haki za binadamu zikiongozwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

Kwa mujibu wa wadau hao, Rais anakusudia kuitoa Tanzania katika wingu lililokuwa limetanda ambalo lilikuwa likikandamiza demokrasia na uhuru wa watu kutoa mawazo. Walieleza kwa kinagaubaga kwamba ni vigumu kwa Rais aliyeko madarakani kufanya mambo kama hayo ambayo yanaweza kusababisha wakati mwingine yeye na chama chake kilichoko madarakani kushindwa.

Miongoni mwa mambo yaliyopendekezwa ni mgombea asitangazwe kupita bila kupingwa na wajumbe wa tume ya uchaguzi wapatikane kwa njia ya wazi kwa kufanyiwa usaili. Muswada pia unapendekeza kuwa badala ya kupita bila kupingwa, apigiwe kura za ndiyo au hapana na kuwe na asilimia ya kura za ndiyo zitakazomthibitisha mshindi.

Sambamba na kupongeza hatua hiyo, wadau waliojitokeza walishauri pia Sheria ya Jeshi la Polisi hususan katika Muswada wa Vyama vya Siasa, ifanyiwe marekebisho kwa kuwa imekuwa kikwazo katika masuala ya kidemokrasia hasa kwenye utoaji wa vibali vya mikutano na suala zima la ulinzi na usalama.


Kwa ujumla, miswada hiyo inakidhi na kujibu baadhi ya mambo yaliyokuwa yakilalamikiwa na wanasiasa kuhusu kukosekana kwa demokrasia hususan uchaguzi huru na wa haki.

Vi vyema wananchi, hususani wapenda demokrasia, wakatumia muda uliotolewa kutoa maoni yao, ama kwa kushiriki midahalo itakayoandaliwa na wadau mbalimbali au kwa maandishi.

Pamoja na hayo, ni faraja kubwa kuwa maoni yatazingatiwa baada ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliyekuwapo katika mjadala huo kusema maoni ya wadau yatazingatiwa. Kwa mantiki hiyo, ni vyema serikali ikazingatia maoni hayo ili kupata sheria zilizo bora kwa maslahi ya Watanzania na kudumisha umoja, amani na mshikamano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tuwe makini na athari za kiafya za mafuriko ya mvua

Na Sabato Kasika

**MVUA** kubwa inaendelea kunyesha mkoani Dar es Salaam na maeneo mengine ya nchi na kusababisha maafa, huku baadhi ya watu wakipoteza mali baada ya maji kuingia ndani ya nyumba zao.

Wengine nyumba zao zimebomoka na kuwaacha hawana makazi, hivyo kujikuta wakiwa katika sintofahamu, huku pia wakikabiliwa na tatizo la kiafya hasa kutokana na maji kujaa katika nyumba zao.

Kwa mazingira kama hayo, ni wazi afya zao ziko hatari, hasa baada ya maji kujaa katika nyumba, maana yake ni kwamba hata vyoo vimefurika maji hayo na kusambaa mitaani na kutishia afya zao.

Lakini maji yakiwa yamejaa kwenye vyoo na kufurika, lakini pia wakati wa mvua kama huu, huwa ni fursa kwa baadhi ya watu ambao hutapisha vyoo vyao ili majitaka yachangamane na ya mvua. Ninadhani wakati huu mvua zinapoendelea kunyesha, ni vyema kuchukua tahadhari ili wasipate madhara ya kiafya, vinginevyo inaweza kuwa rahisi kuvamiwa na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

Yaani waliozoea kutapisha vyoo, waache mtindo huo, lakini pia wale ambao nyumba na vyoo vitajaa maji ya mvua, watoe taarifa kwa wataalam wa afya ili wasaidiwe jinsi ya kujinga na hali hiyo.

Kwa mujibu wa wataalam wa afya, mvua za aina hiyo husababisha utapiamlo, kipindupindu na magonjwa mengine ya kuhara, homa ya matumbo, homa ya ini na malaria.

Ingekuwa ni vyema kama wakazi hasa wa Dar es Salaam, ambao wamekuwa na mtindo wa kutiririsha majitaka wakati wa mvua, waache mtindo huo, ili kulinda afya zao na wengine.

Lakini pia kuna haja ya kujiuliza kwa nini mafuriko yanatokea kila mwaka. "Kwa nini, watu hawajifunzi kutokana na uzoefu na kuchukua hatua mapema za kuepusha janga hilo?

Kimsingi, mafuriko ni moja ya majanga ya asili, lakini wakati mwingine ipo haja kuangalia ujengaji wa nyumba, kwani wapo baadhi ya watu wamejenga kwenye maeneo ambayo maji ya mvua yanapita.

Wakati huu ambao baadhi ya nyumba zimekumbwa na mafuriko, ni muhimu kuchukua tahadhari, kwa ajili ya kuokoa maisha, watu wasijenge katika mikondo ya maji na wasitiririshe majitaka.

Katika mkoa wa Dar es Salaam baadhi ya maeneo ambayo kila mara huathiriwa na mafuriko ni Jangwani, Tandale, Msasani Bonde la Mpunga, Buguruni kwa Mnyamani na Bonde la Mto Kigogo.

Maeneo mengine ni Boko Basihaya na mengine mengi ambayo ni vyema mtu kuuliza kwanza kabla ya kuhamia, kwani hujaa maji ya mvua na kusababisha watu kuhangaika huku na kule kuokoa maisha yao.

Kama nilivyoeleza awali, mafuriko ni moja ya majanga ya asili, lakini ujengaji wa nyumba katika njia za maji ya mvua na msongamano mkubwa wa makazi ya watu imekuwa ni vigumu kwa maji kupita kwenye njia yake na kusababisha mafuriko.

Ukweli ni kwamba kuna athari kubwa za kuzuia njia ya maji, kwani yakifurika huwa hayachagui mahali pa kupita, ndio maana nikaeleza kuwa husababisha mafuriko ambayo wakati mwingine yanaua.

Mvua zikiwa kubwa mito hutapika kwenye kingo zake na kusambaa maeneo ya karibu yake ambayo kwa kiasi kikubwa yamevamiwa na makazi ya watu hivyo ni rahisi kuingia katika makazi.

Mafuriko hayo yanapotokea, huzoa taka za aina, zikiwamo za chooni ambazo ni hatari kwa afya za watu, hivyo suala la kuchukua tahadhari kuanzia ujenzi na hata kutotiririsha majitaka ni jambo muhimu.

## FIKRA MBADALA

# Muswada sheria uchaguzi sawa na mabadiliko ya Katiba bado muhimu



Pascal Mayalla

KAMA kawaida leo nimepata fursa kuwaletea makala elimishi ya uchambuzi wangu wa muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023. Kwa muhtasari wa sura zote 10 za muswada huu, kuwaelimisha elimu ya uraia na elimu ya sheria na haki ili Watanzania tuitumie kikamilifu miezi mitatu iliyotolewa kwa kutoa maoni na mapendekezo kwa ajili ya maboresho ya sheria hii.

Muswada huu unatunga Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2023. Kwa ujumla, sheria hii inaunganisha Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Masharti ya uchaguzi wa Rais na Wabunge na Madiwani ni sheria moja na kutekelezwa na mamlaka moja ambayo ni Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Binafsi, ninapendekeza uchaguzi wote, kwa maana ya uchaguzi mkuu na ule wa serikali za mitaa ufanyike siku moja na kusimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi.

Muswada huu umegawanyika katika sura 10 na nimeamua kufanya uchambuzi wangu wa sura kwa sura na maoni yangu.

Sura ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la sheria inayopendekezwa, mawanda ya matumizi, utaratibu wa kuanza kutumika pamoja na tafsiri ya misamiati mbalimbalikwa kadri ilivyotumika ndani ya Sheria inayopendekezwa. Kwa mujibu wa masharti ya sehemu hii, sheria inayopendekezwa itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa uchaguzi wa Rais na Wabunge na kwa Tanzania Bara kwa uchaguzi wa Madiwani.

Sura hii inajumuisha pia masharti kuhusu ugawaji wa maeneo ya uchaguzi na uteuzi wa watendaji mbalimbali wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambao husaidia kufanikisha shughuli mbalimbali za Tume kama vile uandikishaji wa wapigakura, usimamizi wa uchaguzi na uratibu wa taarifa, upatikanaji wa vifaa, rasilimali na masuala mengine muhimu kwa ajili ya kuendesha uchaguzi.

Miongoni mwa malalamiko, wasimamizi wa uchaguzi ni makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakurugenzi, makatibu tawala wa mikoa na makatibu tawala wa wilaya ambao ndio wasimamizi.

Hawa walikataliwa na mahakama kwenye kesi ya Bob Chacha Wangwe lakini wasimamizi bado ni haohao. Nashauri wawekwe watu ambao hawafungamani na upande wowote au hawana harufu ya ukada.

Sura ya Pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu uandikishaji wa wapigakura. Sura hii imegawanyika katika sehemu nne, ya kwanza inaainisha sifa za mtu kuandikishwa au kukosa sifa za kuandikishwa kuwa mpigakura huku ya pili inahusu Daftari la Awali na Daftari la Kudumu la Wapigakura. Miongoni mwa sifa muhimu za kuandikishwa kuwa mpigakura zilizoainishwa katika Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2023. Sifa kuu ni kuwa raia wa Tanzania na kutimiza umri wa miaka 18.

Sehemu ya Pili inaweka masharti ya uandikishaji ambayo yanajumuisha muda wa uandikishaji, wakala wa uandikishaji, kadi ya mpigakura, utaratibu baada ya mtu kubadili makazi, namna ya kupata kadi mpya endapo ya awali imepotea, imefutika au imeharibika na utaratibu wa uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga Kura ambao unapendekezwa ufanyike mara mbili kati ya uchaguzi mkuu mmoja na uchaguzi mkuu unaofuata.

Sehemu ya Tatu ya Sura hii inaainisha masharti kuhusu utaratibu wa kuweka pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa au dhidi ya jina la mtu kuendelea kubaki katika daftari. Pingamizi dhidi ya uandikishwaji litawasilishwa kwa ofisa mwandikishaji. Sehemu ya Nne inajumuisha masharti kuhusu rufani dhidi ya pingamizi la kuongezwa au kufutwa katika daftari na rufani dhidi ya uamuzi wa ofisa mwandikishaji zitawasilishwa katika Mahakama ya Wilaya.

Kwa moni yangu, kwa vile sifa kuu ni kuwa raia wa Tanzania na kutimiza umri wa miaka 18, bila shurti lingine lolote, hii ndiyo haki kuu ya msingi ya uchaguzi. Ni haki ya kuchagua kwa kupiga kura bila sharti lolote, haki ya kuchaguliwa pia iwe bila shurti la kudhaminiwa na chama cha siasa.

Sura ya Tatu ya Muswada inaweka masharti mbalimbali kuhusu uchaguzi wa Rais na imegawanyika katika sehemu tatu.

Sehemu ya Kwanza, inajumuisha masharti ya uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais, idadi ya wadhamini wanaopaswa kuwa nao na utaratibuwa uchukuaji na urejeshaji wa fomu za uteuzi.

Sehemu hii pia inaweka utaratibu wa namna ya kuweka pingamizi dhidi ya mgombea wa kiti cha Urais na Makamu wa Rais.

Sehemu ya pili ya sura hii inaweka masharti mbalimbali yanayohusiana na taratibu za uchaguzi wa urais ikijumuishasiku ya uchaguzi wa Rais, watu wanaostahili kupiga kura katika uchaguzi wa Rais, sifa za mgombea katika uchaguzi wa Rais, majumuisho ya kura katika uchaguzi wa Rais, mazingira yanayoweza kusababisha upigaji kura kurudiwa na masharti ya kutambulika kwa uchaguzi wa Rais kuwa uchaguzi wa Makamu wa Rais.

Ili kuepuka kurudia masharti kuhusu taratibu za upigaji kura ambazo hufanana kwa uchaguzi wa mgombea wa kiti cha urais, ubunge na udiwani, Sehemu hii inaweka sharti la matumizi ya Sura ya Sita ambayo inaainisha utaratibu wa upigaji kura.

Sura ya Nne ya Muswada inaweka masharti yanayosimamia uchaguzi wa Wabunge na imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya Kwanza inahusu sifa za wagombea katika uchaguzi wa ubunge.

**Wiki ijayo tunaendelea na sura zinazofuata na sehemu kuhusu muswada huu.**

**Mungu ibariki Tanzania**

**Paskali**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Halahala Chifu Manyama jembe lisikatike mpini



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

WASWAHILI waliachiwa na wahenga wao semi nyingi na zote zikilenga kutoa mafunzo na maonyo kwa jamii. Lengo ni kuhakikisha jamii zinaishi kwa amani na utulivu.

Miongoni mwa semi hizo ni kama vile "We ukiona cha nini, wenzio wanajiuliza watakipata lini" au "Jiwe walilolikataa waashi limekuwa jiwe kuu la pembeni" yaani bora na la kuheshimiwa na wengine."

Naweza kuwa sijazipatia kama ilivyo, lakini zinaeleweka na zina maana fulani kwa jamii kwamba unaweza ukawa na kitu ukakiona hakikufai na ukakiponda lakini mwishowe kitakuja kuwa na faida kwa mwingine.

Hiyo hutokea hata katika ndoa ambako watu wanamwona mke wa fulani hafai akiwa naye, lakini kwa wengine anakuja kuwa mke mzuri na mwema pale anapokuwa ameachika.

Siku za karibuni, tumeshuhudia na tunashuhudia kijana fulani hivi aliyetamba huko nyuma akiwa nyuma ya watu wakubwa, akifanya mambo yaliyowashangaza wengi na hata kutuhumiwa kwa ubaya na kupondwa lakini sasa kaibuka upyaaaaa! (Kwa sauti ya Bwege).

Kijana huyo aliyepewa madaraka makubwa, kuna nyakati akajisahau na kufanya yasiyofanywa, tena kwa jeuri na kujikuta akiingia lawamani, ingawa akitenda kulingana na kazi yake na majukumu aliyopewa kwa baraka za mkuu wake.

Si mwingine, bali ni Chifu Manyama, aliyeongoza mkoa mkubwa kwa umaarufu, akaja kujikuta katika lawama za kuvamia kituo cha luninga usiku wa manane na kutaka kulazimisha kichezwe kipindi alichotaka.

Lakini alipotafitiwa na wanahabari fulani hivi, ikabainika alifanya makosa, hivyo kiranja mmoja akasimamia kuanikwa kilichopatikana kwenye utafiti ule. Aliyemteua akasema achana na porojo chapa mzigo.

Na matokeo yake hata kiranja naye hakukaa sana kwenye ukiranja wake, akatupwa pembeni na kujikuta akichapa lapa mtaani, mpaka alipokuja Chifu Hangaya kumwokoa na kumrejesha kwenye ufalme wake ule ule. Wakati hayo yakifanyika ya kurejeshwa kiranja ukiranjani, ndipo Chifu Manyama naye akaibuka na kufanya yake. Anazunguka mkoani huyo kama aliyepagawa, akionekana kuipenda na kuiringia kazi yake mpya ya u-MC wa chama.

Kijana hatulii, hakai sehemu moja! Leo hapa kesho pale. Kila kukicha akihanikiza na viranja wa nchi hii akiwaita kila aliko kuhakikisha kero za wananchi zinasikilizwa na kuchukuliwa hatua ya kuzitatua. Kongole lake Chifu Manyama.

Chifu Manyama hivi sasa ana msafara wa kuua mtu akiwa mkoa fulani utajua tu mkoa umepatwa. Ana maagizo na maelekezo kedekede ya chama, mengine hatukuwahi kuyasikia walipokuwapo waliokuwa na madaraka kama yake.

Kinachonikosha ni jinsi anavyoingia maeneo, leo atapanda bajaji, kesho utamwona kwenye bodaboda na keshokutwa farasi. Bila shaka iko siku kama hatapanda punda basi fisi nao wakae chonjo. Hakika maua yanamhusu.

Hana nia mbaya Chifu Manyama ila anachotaka ni kusikika kuwa kafika na yupo kwa ajili ya maslahi mapana ya wananchi wanaoteseka vijijini na mijini kwa kukosa huduma na mambo mengine ya msingi. Nani basi kama si Chifu Manyama?

Amekwenda mahali ambako kuna wafiwa wamezuiliwa mwili wa mpendwa wao hospitalini kwa sababu tu ya kukosa fedha. Sina shaka waliofanya hivyo, hawakuwahi kumsikia kiranja Ummy akiwaambia "toa maiti malipo baadaye."

Chifu Manyama alilijua hilo fika na kwa kuwa viranja wote hivi sasa akiwamo kiranja mkuu, wako chini yake kwa maagizo ya chama na kwa kuwa ana mapenzi na watu, akatoa agizo la wafiwa kuchukua gari lake na kwenda hospitalini kuchukua mwili wakazike mengine yafuate. Nani kama yeye?

Hakuishia hapo, yakamfikia malalamiko ya maofisa usafirishaji wenye pikipiki zao lupango ya Polisi, wakataka Chifu Manyama afanye awezavyo kuhakikisha bodaboda zao zinaachwa huru ili zikasafirishe wateja.

Chifu huwa hacheleweshi mambo, kama alivyoagizwa na chama, akatoa amri kwa Polisi kuhakikisha bodaboda zote zinazotumikia vifungo mahabusu za nje za Polisi, ziwe huru mara moja na zirejee mkononi mwa maofisa usafirishaji.

Na hiyo ni bila kujali ziko hapo kutoaka na makosa ya ajali, mauaji, wizi au ujambazi, la hasha zitoke na kila ofisa atumie kujipatia kipato, kwa sababu ndilo lengo la chama na Ilani yake kwamba asiyefanya kazi na asile. Polisi sasa hawalali kuzitambua zipi za mauaji, za wizi, ujambazi na makosa mengine.

Hii kasi ya Chifu Manyama, naona kama itakuja kuingia mpaka Magereza ambako itatoka amri kwa maelekezo ya chama, wafungwa watolewe ili wakale maisha uraiani kwa sababu wamekaa sana ndani na huku nje mambo yananoga mtaani.

Sitashangaa kusikia kauli ya watoke ili wakashiriki uchaguzi mwakani na mwaka unaofuata kwa sababu ni wapigakura halali na kufanya hivyo ndiko kutakipa chama fursa nzuri ya kushinda.

Chifu Manyama hoyeee! Nadhani Chifu Hangaya katuletea jembe ila liangalie lisikatike mpini tu!

# Watakiwa kuchangamkia fursa kituo kipya biashara kimataifa

**Na Joseph Mwendapole**

WAFANYABIASHARA wametakiwa kuchangamkia fursa ya vizimba kwenye Kituo cha Kimataifa cha Biashara cha East Africa Commercial & Logistics Center (EACLC) kinachojengwa na Ubungo, Dar es Salaam.

Kituo hicho cha kwanza na cha aina yake kujengwa Afrika Mashariki, kitakuwa na zaidi ya maduka 2,500 na tayari baadhi ya wafanyabiashara wameanza kuvichukua wakisubiri kuanza biashara Juni, mwakani.

Wito huo ulitolewa juzi Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Martin Mbwana, wakati akizungumza kwenye mkutano na wafanyabaishara ulioandaliwa na kituo hicho.

Mbwana alisema kujengwa kwa maduka hayo ni fursa kubwa kwa wafanyabiashara wa Tanzania kwani yatawasaidia kupata bidhaa nyingi kutoka China na kuziuza kwenye masoko mbalimbali ya nchi za Afrika Mashariki.

Alisema yeye ni balozi wa mradi huo na amekuwa akitumia muda wake mwingi kuwaeleza wafanyabiashara wa Tanzania jinsi watakavyonufaika na mradi huo.

"Lazima wafanyabiashara wa Tanzania tujue kuwa hiki ni chuo kikuu kipya cha biashara nchini mimi niko Kariakoo nimebahatika kuishi China na nimeona masoko makubwa yaliyoko kule sasa masoko yale yanakuja nchini tutumie fursa hiyo," alisema.

"Inachofanya serikali ya China ni kupunguza watu kutoka mataifa mbalimbali kwenda kwao wanataka Wachina waje hapa nchini na wamefanikiwa kwa hiyo na sisi tunapaswa kuamka na kuchangamka," alisema.

Alisema Wachina wamechukua maghala mbalimbali nchini ambayo watayatumia kusambazia bidhaa kwenye maduka ambayo yatakuwa kwenye kituo cha EACLC.

Alisema maduka hayo yatakuwa yakiweka bidhaa kama sampuli na mfanyabiashara atakapozihitaji zitatolewa kwenye maghala hayo ndani ya muda mfupi kumfikia mteja.

"EACLC ina uhusiano mzuri na viwanda vya nchini mwao. Kwa hiyo ukishalipia duka hapo kwenye kituo cha Ubungo wanakusafirisha bure kwenda China wanakutembeza kwenye viwanda vyao unatembelea vile viwanda kwa gharama zao unatengeneza mtandao," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa EACLC, Cath Wang, alishukuru namna Watanzania ambavyo wamekuwa wakishirikiana na kampuni yake kwenye ujenzi wa mradi huo tangu waanze kuujenga mwaka huu. Alisema kampuni hiyo imesajiliwa Tanzania na ni muhimu katika kudumisha uhusiano baina ya Tanzania na China huku akisema kuwa wanatarajia mradi kukamilika Juni mwakani na kuanza kufanya biashara. Mbali na maduka hayo, alisema EACLC itatoa pia huduma za usafirishaji wa mizigo kwenye mikoa mbalimbali nchini na hata kwenye nchi jirani.

Meneja wa Kituo cha Uwekezaji (TIC) Kanda ya Mashariki, Fidelis Obanga, alisema ujenzi wa kituo hicho utasaidia sana kupunguza matumizi ya Dola za Marekani katika kuagiza bidhaa nje ya nchi kwani zitakuwa zinapatikana nchini.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amepunguza gharama inayohitajika kwa mwekezaji mzalendo kusajili uwekezaji wake kutoka Dola za Marekani 100,000 hadi Dola 50,000.

"Tunapoongelea gharama za kusajili biashara haina maana kwamba fedha hizo ndizo mwekezaji anapaswa kutoa ili asajiliwe. Hapo tunaongelea gharama nzima za mradi yaani unapotaka kuwekeza angalau uwe na thamani hiyo kuanzia ardhi na vifaa ulivyo navyo, " alisema

Alisema kuna faida nyingi kwa wawekezaji kusajili miradi yao TIC ikiwemo kupata vivutio mbalimbali vya uwekezaji vitakavyomsaidia kuanza uwekezaji. Mary Mwakyosi ambaye ni Mkuu wa Idara ya Viwanda Manispaa ya Ubungo, alisema serikali ilifanya uamuzi mzuri wa kuwapokea wafanyabiashara hao wa China na kuwapa eneo la ujenzi wa mradi wao kwani utakuwa na manufaa makubwa.

Alisema watu wenye makazi maeneo hayo watapata manufaa makubwa kutokana na ukweli kwamba watakuwa wakipokea wageni wengi kutoka mataifa mbalimbali wanaoleta mizigo na wanaokuja kununua.

"Hii ni fursa kubwa kwa wafanyabiashara wa Tanzania na kwa kweli mnapaswa kujiandaa ili mradi huu utakapoanza mchangamkie fursa hizi kuchukua mzigo na kupeleka kwenye mikoa mbalimbali na hata nje ya nchi kwenye masoko mengine," alisema Mary

## TAKUKURU yabaini kasoro miradi ya bil. 4.5/- Ruvuma

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA


TAASISI ya Kuzuia na kupambana na Rushwa Mkoa wa Ruvuma (TAKUKURU) imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi 19 ya maendeleo yenye thamani ya bilioni 4.5 na kubaini kasoro ambazo zimetolewa mapendekezo namna ya kuziboresha.

Akitoa taarifa kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu, Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma, Janeth Haule, alisema tayari miradi iliyokuwa imebainika kuwa na upungufu ilishaanza kufanyiwa kazi na hatua mbalimbali zilichukuliwa.

Haule aliitaja miradi iliyofuatiliwa kuwa ni elimu hasa ujenzi wa madarasa, jengo la utawala na vyoo katika shule nne wilayani Tunduru yenye thamani ya Sh. 911,428,792.16 na Namtumbo ni ujenzi wa madarasa, jengo la utawala na vyoo katika shule nne, yote ikiwa na thamani ya Sh. 849,216,795.42.

Katika Wilaya ya Nyasa, alisema walifuatilia ujenzi wa madarasa, jengo la utawala na vyoo katika shule nne yenye thamani ya Sh. 602,500,000 huku wilayani Songea ikiwa ni ujenzi wa madarasa, jengo la utawala, vyoo pamoja na mabwalo katika shule sita yote ikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. Bilioni 2.2.

Aidha, Haule alisema katika kipindi cha miezi mitatu, TAKUKURU Mkoa ilipokea taarifa 38 kutoka kwa wananchi kupitia vyanzo mbalimbali na malalamiko yote yalifanyiwa kazi. Alisema kati ya malalamiko hayo, 27 yalihusu rushwa na matatu yameshafikishwa mahakamani na kesi zinaendelea.




Mkuu wa usambazaji huduma wa Tigo Pesa, Innocent Mosha (kulia), akimkabidhi wakala wa tigo pesa, Twisila Hillard, mfano wa hundi baada ya kuibuka mshindi wa 'Tigo Pesa wakala push Promo'. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

## Bil. 42/- kutatua kero ya maji Dar es Salaam

**Na Frank Monyo**

SERIKALI kupitia Wizara ya Maji imetia saini mkataba wa Sh. bilioni 42 na kampuni ya SINOHYDRO kutoka China kutekeleza mradi mkubwa wa maji Dar es Salaam Kusini, maarufu mradi wa Bangulo.

Mradi huo utakaosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) unatekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili na unatarajiwa kuwanufaisha zaidi ya wakazi 400,000 kutoka wilaya za Ubungo, Temeke na Ilala.

Akizungumza baada ya kushuhudia utiaji saini jana, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema mradi huo utajibu changamoto ya muda mrefu ya upatikanaji maji katika maeneo hayo pamoja na majimbo ya Ukonga, Segerea, Ubungo, Kibamba na Ilala.

Waziri Aweso aliagiza DAWASA kuongeza nguvu ya kuunganisha huduma ya maji kwa wateja wapya kwa mkopo ili baadaye wakatwe kidogo kidogo.

"Maji hayana mbadala. Maji si kama wali ukikosa utapata ugali. Mtu anayekosa maji madhara yake ni makubwa, hivyo niwaombe DAWASA kuna watu wanaweza kulipa moja kwa moja kuunganishiwa maji lakini vipato tunatofautiana. Kwa kuwa serikali imetoa fedha kwa ajili ya miradi mikubwa, anayeshindwa kulipa muunganishieni na mkateni kidogo kidogo," alisema.

Alisema wakati wa bunge la bajeti, wabunge wa maeneo hayo yanayopita mradi huo waliweka msimamo wakisema bajeti haipiti bila kuingizwa mradi huo kwa ajili ya wananchi wa maeneo hayo.

DAWASA inafanya kazi kubwa ikipata mafua nchi nzima inapata chafya, wizara haitakuwa kikwazo katika kuhakikisha Wakazi wa Dar es Salaam wanapata maji safi na salama," alisema.

lisema wananchi hao wamepata changamoto ya maji kwa muda mrefu hivyo mkandarasi wa mradi huo anapaswa kutekelezwa kwa wakati na kuacha visingizio kwani fedha zipo.

"Jukumu alilo nalo ni kuweka nguvu kazi, kazi ifanyike na ukamilike kwa muda ulipangwa na wasimamizi wa mradi msicheze, msimamieni mkandarasi kwa uaminifu na weledi mkubwa ukamilike na wananchi wapate maji," alisema.

Aweso alimtaka mkandarasi anayetekeleza mradi huo kufanyakazi na kukabidhi mradi kwa wakati.

"Wananchi Hawa wameteseka sana. Mkandarasi huyu asimamiwe kwa uadilifu, hatutaki kuja kisikia mkandarasi huyu amepewa miezi 12 halafu anakuja kuongezewa muda. Mimi ni dogo lakini ni dogo janja. Ukinizingua ninakuzingua," alisema.

Waziri alisema awamu ya kwanza ya mradi huo itanufaisha wananchi wa Kata za Kwembe, Kitunda, Pugu Stesheni, Kipunguni na Mzinga nay a pili itanufaisha wananchi wa kata ya Kivule, Kinyerezi, Zingiziwa, Majohe, Charambe, Kwembe, Buza, Msongola, Msigani na Mbezi.

Mbunge wa Kibamba, Issa Mtemvu, alisema wakati anachukua nafasi hiyo upatikanaji wa huduma ya maji ulikuwa chini ya asilimia 40 na kwa muda mrefu amekuwa akiomba huduma hiyo.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu, alisema wana miradi mingine midogo kama Kibamba ni eneo lenye miinuko mingi wametenga Sh. milioni 500 kwa ajili ya usambazaji wa huduma hiyo.

"Maeneo mengine ni Machimbo, Mpigi Magohe, Mbezi Makabe na Ukonga tumetenga Sh. milioni 200 kuhudumia maeneo ya Bomba Bmbili, Bivule na Pugu Stesheni na sehemu zingine," alisema.

Kingu alisema katika jimbo la Segerea, DAWASA imetenga Sh. milioni 300 milioni ili kujenga vitu vya kusukuma maji kwenye baadhi ya maeneo kama vile Vingunguti na Stakishari.

# MAISHA

NOVEMBA 19, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

**Utamu wa choroko na wali**

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

Yajue matumizi bora ya kona ya nyumba



## 'TAIFA STARS RISING WEAR'


Ukurasa 13




# FURAHIA UREMBO WA ASILI

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| K | ■ | S | I | M | B | A |
| I | ■ | ■ | ■ | W | ■ | M |
| B | ■ | M | I | A | ■ | B |
| O | T | A | ■ | K | U | U |
| N | ■ | N | I | A | ■ | L |
| D | ■ | D | ■ | ■ | ■ | I |
| E | L | E | W | A | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


HAA, MBU, ARA, BAI, ASALI, UGALI, AJABU, HAMIA, IMBISHA, UBWABWA

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI

HAYA, LEO NGOJA TUONE HUWA UNAPATA NGAPI KATIKA SOMO LA KIINGEREZA SHULENI. OANICHA MAJINA NA PICHA ZAKE KWA KUCHORA MISTARI.




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

JAMAA mmoja ambaye ni mara ya kwanza kutembelea mjini, aliwaacha watu hoi kwa kicheko baada ya kupelekwa katika kibanda cha kununulia koni.

**Mama:** Ebu nipatie koni mbili ya kwangu na huyu ndugu yangu

**Jamaa:** Duu, chakula gani hiki mbona kama ko-nokono wa kule shambani, ila huyu ana rangi nzuri

**Mama:** Hapana hii ni koni

**Jamaa:** Tafadhali mama siwezi kula, bora uni-nunulie togwa

**Mama:** Sema taratibu unanitia aibu.

**SWALI**

Tabia za binadamu zinakaribiana na mnyama gani wa porini?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Ulevi unavyodidimiza vijana kimaisha!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuelimishana kuhusu maisha yetu yalivyo kila uchao. Wiki kadhaa sasa nimeelezea roho ya pombe na jinsi inavyotesa watu wengi na hasa vijana katika jamii yetu.

Nikaelezea madhara na vipi wataalamu wanajaribu kulitupia jicho tatizo la unywaji wa pombe kupita kiasi. Pia niliijadili roho hii ya ulevi na jinsi inavyotumika kama silaha ya ibilisi na mawakala wake kuangamiza na kupoteza hatima za watu wengi.

Nilitaja vyanzo kadhaa vinavyosababisha watu wengi kunaswa na roho hii. Uko ulevi wa kurithi hasa wa pombe unaotokana na maagano yaliyowekwa na mababu kwenye ukoo.

Chanzo kingine kuna uchawi wa ulevi wa pombe, bangi, sigara na kadhalika. Mtu anaweza kuwekewa uchawi kwenye pombe na kumfanya ashindwe kuacha pombe. Mtu wa aina hii hufikia hatua ya kutokuwa na akili timamu.

Shetani siku zote amelenga kushusha mafanikio ya mwanadamu na kuharibu kabisa hatima yake. Anajua akimharibu baba ambaye ni kiongozi wa familia, ndoa itasambaratika. Kadhalika pia akifanya hivyo kwa mama nyumbani.

Roho ya pombe hasa unywaji wa kupindukia umeharibu maisha ya ndoa nyingi. Vijana wengi wamejitahidi sana kutengeneza uhusiano wa kuchipua ndoa bora lakini ibilisi wa pombe hakuwapa nafasi ya kushamiri. Wanajikuta ndoto zao hazitimii bali zinaishia njiani.

Wazazi wamejitahidi sana kwa upande wao kusomesha vijana katika ngazi mbalimbali za elimu kuanzia msingi hadi vyuo vikuu. Lakini wako wengi hivi leo wana maumivu rohoni kuona vijana wao walivyoharibiwa na ulevi, hivyo kukatisha ndoto zao.

Hali hii inaweza kuwa imesababishwa na baadhi ya wazazi wenyewe ambao pia ni walevi wazuri wa kupindukia au kama nilivyoeleza awali kuwa asili za watu zimechangia mvurugano huo.

Ni asili kwa sababu hata maandiko ya Mungu yanaonyesha kuwa, "Yaliyokuwako ndiyo yatakayokuwako, na yaliyotendeka ndiyo yatakayotendeka; wala jambo jipya hakuna chini ya jua.

"Je! Kuna jambo lolote ambalo watu husema juu yake, Tazama, ni jambo jipya? Limekwisha kuwako tangu zamani za kale zilizokuwa kabla ya sisi".

Msomaji wangu, kumbe yanayotokea leo, yalishakuwako na yataendelea kuwako. Wako vijana wengi wasomi hata kufanikiwa kupata ajira.

Wanapangiwa nafasi nzuri kazini lakini roho ya ulevi inawavaa, hivyo wanashindwa kuendelea.

Kijana amesoma vizuri, anaoa na kuanza kulea familia ya mtoto mmoja au wawili. Shetani anajichomeka hapo, anatumia wakala wake kwenye maofisi. Wakala anaweza kuwa rafiki yako wa karibu au mfanyakazi mwenzako.

Huyu anakuonea wivu pengine anaitaka nafasi yako. Anakuendea kwa mganga kuvuruga akili yako, anakurushia roho ya ulevi. Anakusogeza karibu mnakunywa wote, kumbe ana jambo katumwa.

Kumbuka adui yako ni yule aliye karibu nawe; rafiki, ndugu, jirani na kadhalika. Siku zote shetani hamshambulii mtu mwanzoni. Husubiri katikati na mwishoni pale mtu anapopata upenyo wa jambo zuri ndipo huzuia.

> **"Wanapangiwa nafasi nzuri kazini lakini roho ya ulevi inawavaa, hivyo wanashindwa kuendelea.**

Nimejaribu kuwahoji vijana kadhaa hasa waendesha bodaboda, nikitaka kujua kwa nini wanakunywa pombe na muda mfupi baadaye wanapakia abiria.

Wengi wanaonyesha kuwa ni kazi inayowaingizia fedha haraka kuliko kazi za ajira kwenye ufundi katika gereji za magari, kushona viatu, vibanda vya chipsi na kadhalika. Pengine kwa tathmini yao ni kweli.

Lakini tatizo langu liko kwenye ulevi wakati wanapoifanya kazi hiyo. Jirani na ninapoishi liko duka moja vijana wa kituo cha kuegesha bodaboda na bajaji huchimbia hapo kunywa pombe.

Si kwamba baada ya hapo hawatakwenda kusaka abiria, la hasa. Watatoka hapo na kurudi kituoni kusubiri abiria. Je, kijana mwenye hali hiyo, akipata abiria wakati pombe ndio iko kwenye mzunguko wa damu, kuna usalama hapo? Hawa ndio wale utawaona barabarani wakijichomeka mbele ya magari wakiwa na abiria, eti wanawahi!

Mmoja kwa jina la Naftali, akasema; mimi mama sinywi pombe nayajua madhara yake. Lakini wenzangu hapa kituoni ni wanywaji, wengine walevi kabisa. Aina ya pombe wanayokunywa sana ni zile kali. Huwaambii kitu!

Bodaboda Dulla anasema: "Lazima ninywe, hela inaingia. Nilikaa sana kijiweni nikawa kibaka. Nilishavuta bangi sana na pombe mbaya. Nilishazoea kunywa. Tena sasa napata hela ndiyo zaidi".

**Msomaji, una maoni? Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Tuache kupuuza wataalam, El Nino imetupa somo

MAAFA yanayotokana na mvua za El Nino zinazoendelea kunyesha hivi sasa katika maeneo mbalimbali nchini, yameacha vilio na simanzi kwa baadhi ya Watanzania.

Wako wenzetu waliopoteza maisha, walioyahama makazi yao bila kupenda, waliozingirwa na maji na wako waliopoteza mali na nyumba baada ya kuharibiwa vibaya na mvua hizo.

Hali si hali. Miundombinu ya barabara maeneo mengi imeharibika vibaya na kwingine mawasiliano yamekatika kabisa.

Hii maana yake nini? hatuna desturi ya kuamini ushauri wa wataalam wetu, hasa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA). Haya yanayojitokeza sasa ni matokeo ya Watanzania kupuuza mambo.

Mikoa iliyoathirika zaidi na mvua hizi ni Dar es Salaam na Tanga. Pia mikoa mingine kama Morogoro na Manyara, ambayo ina miundombinu thabiti ya kukabiliana na mafuriko imekumbwa na adha hiyo.

Kila madhara tunayoyaona sasa ni somo kwetu. Tukiambiwa kuhama mabondeni tuhame. Tuache kupuuza wataalam.

Watawala wamekuwa wapole kwenye hili la kuwaondoa wananchi mabondeni, kisa wanabembeleza kura. Wanaamini kwamba pindi watakapowahamisha, ukifika uchaguzi itakula kwao!

Hatuwezi kufika kwa stahili hii. Kama jambo lina maslahi kwa nchi sawa, kama linaongeza balaa tuchukue hatua na tusipepese macho.

Kuna tathmini ya athari za mazingira (EIA) inayofanywa kisheria na maofisa wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), achilia mbali wananchi wa kawaida, hata taasisi na mashirika ya umma, yanapuuza.

Hawathamini na hawataki kujua kwamba EIA ni mchakato wa kutathmini na kupunguza athari za biofizikia, kijamii na athari zingine zinazofaa za mapendekezo ya maendeleo, kabla ya uamuzi kuchukuliwa.

> **"Hii maana yake nini? hatuna desturi ya kuamini ushauri wa wataalam wetu, hasa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA). Haya yanayojitokeza sasa ni matokeo ya Watanzania kupuuza mambo.**

Iko hivi, kwa wale ambao hatujafuatilia mambo haya ni kwamba tathmini ya athari za kimazingira, hutumiwa mara kwa mara kwa kuwa ina manufaa zaidi katika taifa lolote lile duniani.

Nchi kama nchi, haiwezi kuwa na seti ya sheria na kanuni zilizoendelezwa vizuri, ambazo hazifafanui kwa uwazi au kulazimisha ni shughuli zipi na mambo yapi yanaweza kuruhusiwa.

Kama ndivyo! kuna hatua kadhaa muhimu ambazo kwa ujumla hufuatwa katika mchakato wa tathmini ya athari za mazingira. Moja, kuna kitu hufanyika ambacho hujulikana kama 'screening and scoping' (uchunguzi na upimaji).

Lakini pia kuna 'assesment of environmental risk' (tathmini ya hatari ya mazingira) na kuna kitu kinaitwa 'mitigation' (ushiriki wa wadau) ambao nao hufanywa. Na jambo la mwisho ambalo huzingatiwa na wataalam ni 'monitoring' (udhibiti wa mpango) na 'decision making' (kufanya uamuzi).

Ni makosa makubwa kutotazamwa hatari za ujenzi wa makazi katika maeneo yanayoonekana ni mkondo wa maji.

Kifungu cha 81 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, kinataka utafiti wa tathmini ya athari za mazingira ufanyike kabla ya kuanza au mradi au kutekelezwa.

Huko Tanga, mpaka Kituo cha Afya cha Ngamiani kimejaa maji. Huo ni mfano mmoja wa wazi kuhusu umuhimu wa kuzingatia ushauri wa kitaalam. Ni vyema tukabadilika kifikra na kiakili na kufuata na kuheshimu maoni ya wataalam wetu badala ya kuona ni hadithi au hekaya za abunuwasi. Mzaha mzaha hutumbuka usaha.

• ***Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI



Katibu Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) Baraka Kizuguto na mkewe Milkah Kahema wakiwa na furaha wakati wakifunga ndoa katika kanisa la Mtakatifu Alban, Upanga Novemba 11, mwaka huu na sherehe ilifanyika kwenye ukumbi wa Masiani, Mbezi ya Chini, Dar es Salaam.







# MITINDO



## 'TAIFA STARS RISING WEAR'
## (mitupio ya Taifa Stars)

WENGI wamezoea kuwaona wachezaji wa timu za taifa za nchi za Ulaya wakiingia kambini katika hali ya kipekee na kuibua hisia kwa wananchi wao.

Moja ya kitu cha kufurahisha ni pale tasnia ya mavazi inapohusishwa katika mchezo wa soka na hasa katika kambi za timu zao za taifa.

Kwa mara ya kwanza wachezaji wa tanzania wamejikuta wakipamba vyombo vya habari nchini mara walipoingia kambini kwa kuangaziwa aina ya mavazi waliyotupia.

Hakika inapendeza baada ya mitazamo ya kale ambayo ilikuwa ikichukuliwa ni sawa kwa mchezaji kuvaa hovyo na kuripoti kambini. Sasa hilo halitawezekana kwani suala la mavazi limekuwa kipaumbele zaidi.

Siku zinazokuja wabunifu wa mavazi watapigana vikumbo kuhakikisha wanawavisha wachezaji wa Taifa Star ili kukuza biashara zao na hivyo kuwaongezea kipato wachezaji wetu.

Utakubaliana na hili kwa kuangalia baadhi ya picha ni za wachezaji wa timu ya Taifa Stars waliporipoti kambini na mitupio tofauti ya mavazi.

## UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# FURAHIA UREMBO WA ASILI

PENGINE watu wanaamini kutengeneza ngozi nzuri lazima utumie vipodozi vyenye kemikali vinavyouzwa gharama kubwa, lakini hilo sio sawa na ni kinyume na mtazamo wa urembo.

Unatakiwa kubadili mtazamo huo ambao unapoteza pesa na muda kwa vipodozi ambavyo havikupi matokeo sahihi, bali tumia vyakula vya asili ambavyo vitakusaidia kuwa na mwonekano mzuri kwa gharama nafuu.

**Maajabu ya nazi na urembo**

Tumezoea kutumia nazi jikoni kwenye mapishi, lakini nazi pia inaweza ikatumika kama scrub kwa ngozi yako

Fuata hatua hizi ili kufanya ngozi ya uso wako iwe laini, nyororo na kufanya uso wako kuwa na muonekano mzuri.

Scrub hii unaweza pia kuitumia kwa mwili mzima, lakini kwa leo nitaelezea namna ya kuitumia kwa uso wako.

Wengine huwa wanachanganya nazi pamoja na asali, limao, tangawizi, nk.

Hii ninayoielezea hapa haijachanganywa na kitu chochote kile. Ni nazi pekee

**Jinsi ya kutumia**

Andaa nazi yako kwa kuikuna vizuri. Ili upate matokeo mazuri jitahidi kuikuna taratibu ili itoke laini.

Safisha uso wako kwa maji safi na sabuni ya kawaida.

Kausha uso wako kwa taulo safi na baada ya kukauka, chukua ile nazi yako uliyokuna tayari, taratibu anza kusugua usoni kwa dadika kama tatu mpaka tano

Ukishamaliza hapo, utakaa hivyo bila kuuosha uso wako kwa muda wa dakika 15 mpaka 20.

Baada ya muda huo, utaosha uso wako kwa sabuni ya kawaida.

Kausha uso wako kwa taulo safi, kisha paka losheni yako unayotumia siku zote.

Ili kupata matokeo mazuri fanya hivi kwa muda wa siku tano mfululizo bila kuacha, yani mara moja kwa siku. Utapata matokeo mazuri.





## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Utamu wa choroko na wali

CHOROKO ni mboga ambayo inatumika kupikwa yenyewe au kuchanganya na vyakula vingine kama mchele, ndizi na viazi.

Choroko zinawahi kuiva tofauti na maharage au nafaka nyingine, lakini pia zinavimba.

Leo tutaelekezana namna ya kuzipika choroko kwa kuunga na nazi na ukala na wali au chakula kingine utakachopendelea.

**Mahitaji**

Choroko kikombe kimoja na nusu, nazi kopo moja, kitunguu maji kimoja kikubwa, nyanya 1/2 kopo na kitunguu swaum kimoja cha chai.

Mahitaji mengine ni Curry powder kijiko cha chai chumvi kiasi, olive oil na pilipili nzima

**Namna ya kuandaa**

Loweka choroko usiku kucha kisha zichemshe mpaka ziive na ziweke pembeni.

Baada ya hapo saga nyanya, kitunguu maji na swaum kisha vipike mpaka maji yote yakauke.

Baada ya hapo tia mafuta na curry powder, pika mpaka nyanya zitoe mafuta kisha tia choroko, tui la nazi, maji nusu kikombe, pilipili na chumvi.

Anza kukoroga taratibu na uache ichemke. Pika mpaka tui la nazi litakapoiva na rojo ibakie kidogo, kisha ipua na mboga yako itakuwa tayari kwa kuliwa.







## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# YAJUE MATUMIZI BORA YA KONA YA NYUMBA

KILA kona ya chumba iliyo tupu ni fursa yako kubuni namna ya kuipendezesha.

Wakati unaipendezesha una fursa ya kuitumia pia hata kama awali ilikuwa inaonekana haiwezi kufaa kwa matumizi.

Ziko njia nyingi za namna ya kubuni kutengeneza kona yako ikapendeza na hata kupendezesha nyumba yako pia.

Njia mojawapo unaweza kuamua ukaitumia kama shubaka la kuhifadhia vitabu vyako kwa kuitengeneza kufuatisha muundo wa kona.



Hii ni moja ya njia nzuri kufanya kona isiyokuwa na kitu itumike na shubaka linaweza kutengenezwa kwenda juu karibu na dari kulingana na mahitaji na ukubwa wa kona ya nyumba yako.

Mbali na shubaka la vitabu, pia unaweza kutengeneza kona yako kwa ajili ya kuweka mapambo madogo madogo. Pia kona inatumika kutengeneza sehemu ya kufanyia shughuli mbalimbali za kiofisi au kusomea.

Kumbuka sehemu ya kona ikitengenezwa vizuri, ni nzuri zaidi na hutuliza akili hususani kwa wanaosoma.

Pia unaweza ukaitumia kona kama sehemu ya kutundika picha za familia. Huhitaji ukuta mkubwa kwa ajili ya kusambaza picha za familia yako badala yake tumia kona hiyo kuongeza mvuto na pia usiweke nyingi zikakuharibia mvuto.

Pia kuweka ua la mmea wa kuoteshwa endapo hutataka kuweka shelfu au sanaa zozote na itasaidia kuingiza uoto asili ndani ya nyumba kwa sababu matawi yake yatatosha kuijaza kona yenyewe.

Kwenye chumba, kona hiyo unaweza kuitengeneza vizuri kama sehemu ya kutundikia nguo hasa kwenye chumba cha kunyooshea au kinachotumika kwa ajili ya kulala.

Hata katika chumba cha wageni ambacho mara nyingi huwa si kikubwa, unaweza kuitumia kupachika hata ubao mwembamba unaoweza kukutanisha pande zote mbili za kuta na hapo ukatundika nguo zako na zikakaa katika mwonekano mzuri.

Na kwa wenye sebule au vyumba vyenye nafasi ndogo, kona inafaa pia kuweka sofa hasa ya duara yenye vipande viwili ambavyo vinaunganika.

Pia unaweza kupendezesha kona yako kwa kuweka vinyago ambavyo navyo lazima uweke juu ya meza ndogo au ukapatengenezea kabati au meza ya miguu mitatu.

Ni vizuri zaidi ukimtumia fundi kukufanyia dizaini ya namna ya kutumia kona yako kulingana na kitu utakachoona kitaipendezesha zaidi.

## Tumia glasi kubadili mwonekano wa nyumba yako

**Na Restuta James**

WIKI iliyopita nilikukumbusha mambo ya kuzingatia ili uweze kubadili mwonekano wa nyumba au madhari ya nyumbani mwako katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Msomaji wangu aliyejitambulisha kwa jina la Regina Joshua, alinipigia simu na kunipa mbinu nyingi zaidi za namna ya kupamba nyumba hata baada ya sikukuu za mwisho wa mwaka.

Anasema glasi za mvinyo ni pambo zuri katika kubadili mwonekano kwa kutumia kufunika aina fulani za pambo ili kunogesha meza au korido.

Anasema kwa wakati huu wa sikukuu, aina hiyo ya glasi inaweza kutumiwa kufunika vimipira vilivyozoeleka kupamba mti wa Krismasi na kuongeza mvuto.

Regina anasema juu ya glasi iliyofunikwa (kama inavyoonekana pichani), unaweza kuweka mshumaa mkubwa unaotosha kwenye mzunguko huo.

"Mshumaa unatakiwa uenee juu ya glasi. Unaweza kuweka mshumaa mweupe usio na manukato au ukaweka wenye harufu nzuri kadiri utakavyoona inafaa," anasema.

Anasema glasi zinaweza kufunikwa juu ya 'table mats' au kwenye trei nzuri na inapendeza zikiwekwa kwenye meza ya console au kwenye shelfu ya kuwekea picha koridoni.


Anashauri kuwa ukubwa wa glasi ndio utakaoamua aina ya mapambo na kwamba kwenye trei unaweza kuweka pambo lingine kadiri unavyoona inafaa.

"Glasi zisiwe nyingi wala isiwe moja. Nne ni standard kabisa lakini hata tatu zinakaa vizuri. Si lazima ununue mapambo ya gharama kuifanya nyumba yako classic. Glasi ulizonazo ukizitumia vizuri unaokoa gharama na unaonekana wa kisasa," anaongeza Regina.

Tuwasiliane kupitia 0753 333 330 au restutajames@gmail.com.



# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... HATA SHERIA INAKUFUNGA LAKINI HAINA GOLI...

## HABARI KIMATAIFA

# Rais George Weah akubali kushindwa

**MONROVIA,** LIBERIA

MATOKEO ya uchaguzi wa Liberia duru ya pili imemthibitisha mgombea wa upinzani Joseph Boakai ameshinda kwa kupata asilimia 50.89 na kumuangusha Rais George Weah.

Rais Weah amempigia simu Boakai kumpongeza kwa kupata ushindi huo. Katika hotuba yake kwa taifa Rais Weah alisema watu wa Liberia wamezungumza na wamesikia sauti yao.

Boakai anaongoza kwa kura 28,000 wakati kura zote zikiwa zimehesabiwa.

Nyota wa zamani wa kandanda, Rais Weah amekuwa madarakani tangu 2018 na atamaliza muda wake Januari mwakani.

Alipoingia madarakani alikuwa akiungwa mkono na vijana na kumshinda mpinzani wake Boakai kwa tofauti kubwa ya kura.

Hata hivyo, analalamikiwa kwa kushindwa kukabiliana na ufisadi, kupanda kwa gharama ya maisha na kuendelea kwa matatizo ya kiuchumi na kuharibu sifa yake.

Rais Weah alikubali kwa hekima kuwa ameshindwa, wakati akianza hotuba yake ya dakika tano na kueleza anaheshimu sana mchakato wa kidemokrasia ambao umelifafanua taifa hilo.

Aliongeza kwamba alizungumza na Boakai ambaye alimwita rais mteule.

Hapo awali tume ya uchaguzi ilitangaza kuwa Boakai, ambaye ni mkongwe wa kisiasa mwenye umri wa miaka 78 alikuwa na asilimia 50.89 ya kura, huku Rais Weah akiwa na 49.11.

Rais alifafanua kwamba ukaribu wa kura katika kinyang'anyiro hicho unafichua mgawanyiko ndani ya nchi na kutoa wito kwa Waliberia kushirikiana kutafuta muafaka na umoja ambacho ni muhimu kwa taifa hilo.

Wafuasi wa rais mteule Joseph Bokai wamepokea ushindi wa mgombea wao kwa shangwe.

Hata kabla matokeo ya mwisho kutangazwa, tayari walishaanza kuingia katika mitaa ya jiji kuu la Monrovia na kushangilia.

Wafuasi wengi zaidi walikusanyika katika makao makuu ya chama chao wakiimba kwa furaha na kumtaka Rais George Weah aliyeshindwa kwenye kinyang'anyiro hicho kukubali kubwaga manyanga.

Wengi wao walikuwa wakiimba kuwa "tumemshinda mcheza densi la Buga" wakimaanisha Weah ambaye kampeni yake ilipambwa na kibao Buga kilichoimbwa na msanii Kizz Daniel kutoka Nigeria.

**BBC**



Uharibifu uliofanywa katika ukanda wa Gaza baada ya mashambulizi ya ndege ya Israel. **PICHA: AP**

# Israel yawataka Wapalestina wanaoishi kusini kuhama

**TEL AVIV,** ISRAEL

ISRAEL imetoa onyo jipya kwa raia wanaoishi Gaza kusini katika kitongoji cha Khan Younis kuondoka.

Onyo hilo limekuja siku tatu baada ya jeshi la nchi hiyo kuangusha vipeperushi vya kuwaonya watu kuondoka eneo hilo.

Khan Younis ndio mji mkubwa zaidi kusini mwa Gaza ambao wanaishi maelfu ya watu waliokimbilia baada ya kuambiwa wahame kaskazini.

Huku mzozo wa kibinadamu ukizidi kuwa mbaya katika jiji hilo lililojaa watu wengi, onyo la Israel lilidokeza kwamba operesheni za kijeshi ziko karibu.

Mark Regev, mshauri wa Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, aliviambia vyombo vya habari vya Marekani kuna wakati wanajeshi wa Israel watalazimika kuingia mjini humo kuharibu mahandaki ya Hamas, watu wa Khan Younis wanaweza kuhamia magharibi ambako kutakuwa na mahema na hospitali.

"Nina hakika kwamba hawatalazimika kuhama tena" ikiwa watahamia magharibi, alisema.

Mamia ya maelfu ya watu wa Gaza walikimbia kaskazini kuelekea maeneo ya kusini ikiwa ni pamoja na Khan Younis baada ya kuamriwa kuondoka na Israel kwa usalama wao.

Lakini eneo la kusini limeendelea kuwa chini ya mashambulizi ya Israel.

Katika hatua nyingine, Israel ilisema itaruhusu malori mawili ya kubeba mafuta kwa siku kuingia Ukanda wa Gaza.

Ofisa wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani alisema takriban lita 140,000 za mafuta zitaruhusiwa kuingia Gaza kila baada ya siku mbili.

Mafuta mengi yatatumiwa na lori ya Umoja wa Mataifa zinazopeleka misaada ya kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira.

Mafuta mengine yatatumika katika kuendesha huduma za simu na mtandao, ambazo zimekatika kutokana na ukosefu wa mafuta.

Juzi kampuni inayotoa mawasiliano ya Gaza ilisema kuwa huduma zake zilikuwa zikirejea baada ya kupokea mafuta kupitia shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi wa Kipalestina.

Ofisa huyo wa Marekani alisema nchi yake ilitoa shinikizo kubwa kwa Israel kufikia makubaliano hayo.

**BBC**

# Tetemeko laua saba Ufilipino

**MANILA,** UFILIPINO

IDADI ya watu waliofariki kutokana na tetemeko la ardhi lenye nguvu kuipiga kusini mwa Ufilipino imeongezeka na kufikia saba.

Juhudi za uokoaji zinaendelea kuwatafuta watu wawili wanaohofiwa kufukiwa kufuatia maporomoko ya ardhi.

Tetemeko hilo lenye ukubwa wa 6.7 lililikumba eneo la Mindanao mchana wa juzi na kusababisha sehemu ya paa la duka moja kuporomoka, kukatika kwa umeme na watu kukimbilia mitaani.

Kulingana na polisi, vifusi vya duka hilo katika mji wa General Santos vilipelekea kifo cha mwanamke mmoja. Waokoaji walisema tetemeko hilo lilisababisha uharibifu wa nyumba 60 katika mikoa minne pamoja na barabara na madaraja 32 katika eneo hilo.

# Majeshi Sudan yalaumiana kwa kushambuliwa bwawa

**KHARTOUM,** SUDAN

JESHI la Sudan na wanamgambo wa Rapid Support Forces (RSF) wamelaumiana kutokana na shambulizi lililoharibu daraja katika bwawa la Jebel Awlia kusini mwa Khartoum.

Ukubwa wa uharibifu uliofanywa katika bwawa hilo bado haujabainika ila uharibifu ni mkubwa ambao unatishia kusababisha mafuriko.

Hivi karibuni mapigano yameongezeka katika eneo la Jebel Awlia, ambayo ni wilaya ya kimaskini kusini mwa jimbo la Khartoum na kusababisha maelfu ya watu kuachwa bila makazi.

Mapema mwezi huu RSF ilisema imeiteka kambi ya jeshi katika eneo hilo.

Katika wiki za hivi karibuni, daraja moja katika Mji Mkuu wa Khartoum na hifadhi muhimu ya mafuta viliharibiwa kwa mashambulizi na pande hizo mbili.

**DW**

## MAKALA

# BIMA YA AFYA TUSIKAMATANE UCHAWI



Na Magabilo Masambu

**Wako baadhi ya viongozi wanasema watu wapewe elimu kuhusu bima ya afya kwa wote ili wajiunge. Jambo hilo ni sawa lakini naona wanaotakiwa kupata elimu zaidi ni watoa huduma ili wakiweza kuwathamini na kutoa huduma nzuri kwa wanufaika, hilo pekee litakuwa kivutio kwa watu wengi kujiunga bila shida. Hata migahawa inayijaza watu wengi mijini ni ile inayohudimia vizuri kuanzia kwenye kauli za wahudumu wao.**

PAMEKUWEPO na mwendelezo wa mjadala kuhusu bima ya afya kwa wote. Baadhi ya wananchi wakionyesha kukubalina na wengine kutokukubaliana na bima hiyo ya serikali.

Ni kweli kwamba bima ya afya ni muhimu kutokana na udharura wa kuugua kwa maana kwamba ugonjwa si sherehe ambayo mara nyingi watu hujiandaa kwa muda mrefu, wenyewe haupigi hodi ni wakati wowote unatokea kwa maana hiyo, lazima pawapo na maandalizi pia ya wakati wowote kukabiliana na changamoto hiyo.

Ukisikiliza maoni ya baadhi ya viongozi kuhusu mtazamo wao juu ya bima ya afya kwa wote, ni kama wanawashangaa wananchi kushindwa kukubaliana mara moja na jambo hilo. Ukisikiliza upande wa wananchi pia, yako malalamiko ambayo kimsingi ndiyo yanayoibua mjadala wa ama wakubaliane au wasikubaliane na mpango huo wa serikali. Lakini ukitazama picha kubwa ya jambo hili nia na kusudio laweza kuwa jema, mashaka ya wananchi ni juu ya utekelezaji wake na hasa eneo la huduma yenyewe.

Hakuna mtu asiyetaka kupata huduma ambazo hazitokani moja kwa moja na fedha yake. Kila Mwananchi angependa kupata huduma ambayo inazidi kiwango cha matumizi ya fedha yake kwa maana kwamba kama kila mmoja atakuwa mwanachama katika bima ya afya kwa wote. Wako watakaonufaika na mpango huo zaidi ya kiwango watakachochangia jambo ambalo ni zuri lenye kusaidiana.

Lakini utafiti mdogo niliyofanya kwa kufanya mazungumzo na baadhi ya wanufaika wa bima zilizopo sasa, ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) hasa kwa watumishi wa umma, wengi wanalalamikia huduma zisizoridhisha na utaratibu uliotumika katika kupanga wategemezi kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya, Sura 395 ya mwaka 2015 na kanuni zake za mwaka 2002.

Mapendekezo ya muswada huu wa bima ya afya kwa wote umekuwa na utaratibu ule ule wa mfuko wa bima ya afya ya sasa kumchagulia mchangiaji wategemezi ambao wametamkwa moja kwa moja, badala ya kumwachia mchangiaji uhuru wa kupendekeza mtegemezi kutokana na uhitaji. Maana yangu ni kwamba, iwapo wategemezi waliotamkwa kwenye sheria hawapo basi mchangiaji aweke wali-opo badala ya kukatwa michango yake na huku akilazimika kuingia mfukoni kutoa fedha za kuwalipia ambao wangeweza kuingizwa kwenye mfuko.

Mfano, sheria inataka mtegemezi awe wazazi, watoto, mwenza au wazazi wa mwenza kama mchangiaji hana wazazi labda wameshatangulia au hakulelewa kabisa na wazazi pengine alilelewa na bibi, basi awe na uwezo wa kumwingiza bibi kwenye mfuko wa bima kama mtegemezi halali. Kwa hiyo, kuunda mfuko wa bima kwa kutumia taratibu zile zile za mifuko ya sasa ambayo haijaondoa malalamiko ya wananchi ni kuandaa malalamiko mengine makubwa zaidi huko mbele.

Eneo la pili ni huduma yenyewe. Pamekuwapo na malalamiko ya waziwazi kuhusu namna wanufaika wa bima ya afya wanavyotazamwa na kuchukuliwa wawapo kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya kama hospitali au vituo vya afya. Wamekuwa wakionekana kama watu wasiothaminiwa kuliko wale wanaotoa pesa taslimu.

Wakati mwingine kuna baadhi ya huduma hazitolewi kutokana na aina ya bima walizo nazo, jambo ambalo si rahisi kueleweka kwa haraka maana anachojua mchangiaji ni kwamba anakatwa fedha kila mwezi, lakini haumwi kila mwezi na bado ataambiwa aina fulani ya huduma haistahili kutokana na aina ya bima anayotumia.

Wako baadhi ya viongozi wanasema watu wapewe elimu kuhusu bima ya afya kwa wote ili wajiunge. Jambo hilo ni sawa lakini naona wanaotakiwa kupata elimu zaidi ni watoa huduma ili wakiweza kuwathamini na kutoa huduma nzuri kwa wanufaika, hilo pekee litakuwa kivutio kwa watu wengi kujiunga bila shida. Hata migahawa inayijaza watu wengi mijini ni ile inayohudimia vizuri kuanzia kwenye kauli za wahudumu wao.

Ushauri wagu kwa serikali ni kwamba kuna kila sababu ya kuchukua hatua kali za waziwazi kwa watoa huduma, wanaowahudumia wanufaika wa bima ya afya na ikiwezekana kila kituo cha afya na hospitali pawapo namba za simu ambazo wananchi wanaweza kutoa taarifa moja kwa moja sehemu husika, badala ya kutumia masanduku ya maoni ambayo wenye funguo ndio wanaolalamikiwa.

Pamoja na hatua kali kuchukuliwa pia wanapaswa kupewa elimu ili kujua kwamba mishahara minono wanayolipwa inatokana na michango ya wanachama. Kwa hiyo hawatakiwi kuwafokea au kuwadharau mabosi wao waliowaajiri kupitia michango kwenye mfuko.

Naamini kwamba changamoto zilizopo sasa NHIF zikipata majawabu na si majibu, basi yatasaidia kuboresha mfuko mpya wa bima kwa wote na kila mtu atasikia fahari kuwa miongoni mwa wanufaika bila kulazimishwa au kutishwa wala kuzuiwa kwa baadhi ya huduma kama kadi za NIDA, leseni za magari na kadhalika. Wananchi hawana tatizo iwapo watahakikishiwa huduma bora. hivyo hakutakuwa na mchawi zaidi ya sisi wenyewe katika jambo hili.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar-es salaam-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Muuza chips aliyehamishwa kitongoji kwa tabia ya kurubuni wake za watu*



Na Adam Fungamwango

KUNA watu wakitaka kukutafutia zengwe bwana hawashindwi. Na usiombe kama jamaa wenyewe wana uwezo wa kifedha, yaani wanajiweza.

Kwa mwenye pesa lolote linawezekana kwa sababu hata mwanamuziki Marijani Rajab, aliimba kuwa pesa inaweza kuvunja mabonde na milima kwenye wimbo wake wa 'Pesa Sabuni ya Roho.' Anamaanisha kwamba mwenye pesa anaweza kuuondoa mlima, akalipa watu pesa na makatapila yao wakauvinjilia kwa mbali.

Maana halisi hapo ni kwamba yeyote mwenye pesa anaweza kufanya lolote, wakati mwingine hata kuvunja sheria na iwe ngumu sana kumkamata. Hata akikamatwa kutiwa hatiani inakuwa na ugumu wake. Anaweza kutumia uwezo wake wa kifedha hata kuwaweka mfukoni baadhi ya watu waliopewa wajibu wa kusimamia sheria, taratibu na kanuni.

Mwanamuziki Patrick Balisidya naye aliimba kwenye wimbo wake aliouita 'Pesa', akisema binadamu anasumbuka na kitu kinaitwa pesa ili aheshimike na imeua watu wengi sana kwa sababu wengine wanaitafuta kwa njia haramu.

Mwanamuziki mwingine Lovy Longomba katika wimbo wake wa 'Pesa' akiwa na Super Lovy, alikuwa anamuuliza pesa ameumbwa na nani? Mbona anasumbua akili za watu. Akamalizia kushangaa kuwa binadamu akipata pesa shida, akiikosa taabu.

Hata Kalala Mbwembwe akiwa na Orchestra Super Sound kupitia wimbo wa 'Fanta', alizungumzia namna pesa inavyoweza kumfanya asiye na fedha akanyanyaswa. Anaelezea mpenzi wake Fanta alivyomkimbia kwa sababu hakuwa na fedha na kwamba mwenye fedha katumia 'uchawi wa kizungu' kumpoka mrembo huyo.

Wakati mwingine pesa inaweza kumfanya mtu kuwa limbukeni baada ya kuzipata. Ndiyo maana baadhi ya watu baada ya kupata tu fedha, wanaanza kufanya mambo ya ajabu hata wengine kuwasababishia kifo. Hamza Kalala katika wimbo 'Pesa' alioimba na kundi na The Bantu Group anasema "Pesa zinanipeleka mbio". Anahoji una mke na watoto kimada wa kazi gani?

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, maeneo ya Mwananyamala, vibopa au mashefa wakati huo wenye pesa wakiitwa, kwa sasa mapedeshee au wafadhili, kwa kutumia pesa zao waliungana kumhamisha kijana mmoja muuza chipsi.

Kwa hali ya kawaida, hakuna mtu yoyote hapa Bongo au sheria inayompa mamlaka ya kumfukuza, kumtoa au kumhamisha mtu kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Sheria ya nchi ni kwamba Mtanzania yeyote atakaa popote ili mradi tu havunji sheria za nchi na si kwa matakwa wa watu binafsi.

Lakini pesa ilisababisha kupindishwa kwa vitu vyote hivyo, hata mamlaka za kiulinzi na serikali yaa mtaa zikapindisha na kubariki kutimuliwa kwa kijana yule muuza chipsi. Kisa ni nini?

Mitaa ya Mwananyamala A kuliwa na kijana aliyekuwa anapika na kuuza chipsi.

Zilipendwa na watu wengi, hasa kinadada na kinamama, ambao walimiminika kuanzia jioni hadi usiku kununua chipsi zake.

Kilichotokea ni kwamba wanawake walioonewa wakanogewa na chipsi hizo kiasi kwamba wakawa hawataki kupika majumbani mwao. Wao chakula chao ni chipsi tu, tena kijana alikuwa anauza bei poa.

Wanaume wengi hakawa hawapikiwi chakula hasa usiku. Sasa wale wanaume wenye uwezo wa kipesa wakakutana ili kupanga mikakati wa kufanya. Wamfanyeje muuza chipsi? Wamuue? Haiwezekani!

Kikao kikafanyika ukumbini kabisa kama cha harusi vile. Kilichoamuliwa ni kumtimua aondoke na asifanye biashara Mwananyamala yote. Wengine wakasema kama atauzia Kinondoni au Tandale, wake zao watakwenda kwa sababu ni karibu.

Basi likapikwa zengwe na kwa kutumia pesa. Pesa ni mwanaharamu siku zote, watu wa mamlaka wakapenyezewa rupia, kama Marijani Rajabu alivyosema penye udhia penyeza rupia, wakamtimua kijana yule. Si kuhamishwa Mwananyamala tu, hata Kinondoni asifike kabisa, kisa eti ni kurubuni wake za watu.

Likapachikwa kosa la kurubuni wake za watu ili liwe zito, yaani anatembea nao kimapenzi, maana wakisema wanawake wananunua sana na hawawapikii waume zao litaonekana halina nguvu.

Ndivyo muuza chipsi alivyofukuzwa Mwanyamala. Wa kumlalamikia hakuna. Siku moja akakutana na mwanamuziki wa Bicco Stars, marehemu Ramadhani Kinguti, akamsimulia kisa.

Kinguti kwa kumsaidia kufikisha ujumbe akakitungia wimbo kikaitwa 'Muuza Chipsi'. Ngoja nikupe mashairi machache ya wimbo huo ambao ulikuwa maarufu.

"Mimi sisemi tena, yaliyonisibu ni makubwa, mimi sisemi tena. Nimekaliwa kikao cha kuhamishwa Mwananyamala, hata Kinondoni nisifike kabisa, kisa ninarubuni wake za watu."

Hiki ndicho kisa cha muuza chipsi ambacho kilisababisha bendi ya Bicco Stars chini ya Kinguti. System ikafyatua kibao hicho kilichotikisa mno miaka hiyo.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Kafie Kwenu-20

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

*************************************

ULINIKATAA sawa, lakini kwa kunibeza, kunidharau, kunidhalilisha na kuninyanyasa. Kwa hili siwezi kwa sababu hata nikikubali na kukaa na wewe sitoweza kusahau. Litaendelea kukaa kichwani kwangu milele hata tukiwa mke na mume.” Akajibu James huku Carry akiangua kilio.

“Nisamehe sana Carry kwa hilo, huna haja ya kulia, mimi nilikusamehe kitambo tu, kuwa na amani mimi si mtu wa visasi. Nitaendelea kuongea na wewe na kusalimiana, kupiga stori popote tutakapoonana, na kukusaidia kwa chochote utakachohitaji, hata kama utataka kazi kwenye makampuni ya baba yangu aliyoyaacha, ila ambacho sitoweza ni kuwa tena mke au mpenzi wako.”

“Jamani James binadamu tumeumbiwa makosa, nisamehe nimekosa mwenzio.”

“Nimekwambia nimekusamehe kwa kila kitu, lakini siyo kuwa mpenzi wako wala mumeo kwa sababu tayari yupo ninayempenda.”

Jibu hilo lilionekana kumtia wazimu Carry na akagaragara chini huku akiendelea kulia. James alimwangalia Carry kwa huruma iliyochanganyikana na kiburi kidogo.

“Kusema kweli nilivyokuona kwa mara ya kwanza ulijaa moyoni mwangu, lakini kila siku zilivyozidi kwenda mbele, mambo ulionifanyia mapenzi juu yako yalikuwa yanapungua taratibu hadi yakaisha kabisa ila wewe ulikuwa hujui, uliendelea kuniona mpuuzi.”

Carry aliona sasa hawezi kumshawishi James kwa lolote kwa sababu ametumia mbinu zote za kuomba radhi lakini ilishindikana.

James alizidi kutazama, mawazo yakamrudisha mbali sana, enzi zile alizokuwa akiishi kwenye kijumba kidogo kule chini.

“Hivi kama nikikukubalia kikaragosi wewe, utanipa nini? Hivi unavyojiona.Umeniona mimi nilivyo? Hivi unaweza kunihudumia ikiwa wewe mwenyewe tu huwezi kujihudumia hapo ulipo.” Akakumbuka moja ya kejeli zake huko nyuma. Bado akaendelea kukumbuka alivyonyanyaswa huko nyuma.

“Ngoja nikwambie kitu, wewe ni mwanamke mrembo sasa, naamini ni wanaume wengi wanakupenda na wenye uwezo kuliko mimi...

“Wenye pesa zao na mali zao, ongezea hilo.” Akamkatisha.




**“Kwa mapishi yale. Wali samaki mbichi, bamia, nyanya chungu, sijui na nini, weee.” James alisababisha Catty kucheka hadi machozi yakamtoka. Baada ya kutulia, James akiwa ametulia, akamwambia Catty.**

“Ni kweli nafahamu hilo.”

“Enhee, sasa mbona unajitia uhayawani!”

“Siku zote mapenzi na pesa ni vitu tofauti. Mapenzi yanatakiwa kwanza yaanze halafu pesa inarutubisha, lakini pesa haiwezi kuanzisha mapenzi...”

“Naona siku hizi we bwana umekuwa mtunzi mzuri wa nyimbo, tafuta mfadhili au mdhamini akupeleke studio, utatoka rafiki yangu ili uondokane na hali uliyonayo.”

“Narudia vil vile kukwambia Carry kuwa nakupenda.”

“Koma wee usiniletee uchuro hapa. Kwanza ishakuwa mkosi, na safari yangu niliyoipanga kwenda siendi tena, naweza kupata majanga makubwa kuliko haya, ngoja nirudi zangu tu nyumbani.”

“Poa, kwaheri Carry.”

Ni moja kati ya mazungumzo aliyoyakumbuka miaka zaidi ya miaka miwili na nusu iliyopita yaliyomkwaza kutoka kwa Carry.

Jinsi Carry alivyokuwa akijiliza, ndivyo James alivyozidi kukumbuka madhila.

Akakumbuka jinsi alivyopigwa na ugonjwa wa malaria na UTI na kushindwa kufanya kazi yoyote kwa zaidi ya mwezi mmoja, lakini akafadhiliwa matibabu na chakula na Catty kwenye nyumba ile ambayo leo yumo. Akakumbuka pia jinsi Carry alivyoendelea kumsimanga alipokuwa akija kula chakula.

“Unafikiri sijui, unaumwa, hela huna, huna pesa ya matibabu, huna pesa ya kula, kwa hiyo hapa ndiyo umeona sehemu ya kuja kuugulia. Yaani hapa ndiyo wodini, hotelini, halafu ndiyo unanitaka mimi.”

“Sasa si ningekuwa na mzigo tu hapa, mtu anaumwa hata pesa ya matibabu inakushinda.”

Unataka uwe unakuja hapa kula huku unaumwa halafu ukizidiwa utufie tupate kazi ya kusaka ndugu zako ambao hatuwafahamu. Kafie kwenu.” James akazidi kukumbuka na neno la mwisho la ‘Kafie Kwenu’, lilimkera zaidi.

Akakumbuka pia alivyokaa na Catty ambaye alimpa ushauri wa kuachana na Carry na sababu hakupenda jinsi anavyomdhalilisha.

“Usihangaike na mtu asiyekupenda siku zote. Carry ni sistaduu, hawezi kuwa na mwanaume kama wewe, anataka wa hadhi ya juu kama mwenyewe alivyo. Na siyo yeye tu, wasichana wengi wa kisasa ndivyo walivyo.

Tafuta wa saizi yako. Usipende kudhalilishwa na kila mwanamke unayekutana naye barabarani. Kuna wengine watakukataa kistaarabu lakini wengine watakudhalilisha kama anavyokufanya dada yangu.

“Endelea kumtafuta utampata tu na wala hutotumia nguvu kubwa sana kumpata, ndege wa rangi moja huruka pamoja.” Akaukumbusha ushauri ambao aliupigilia msumari na akaanza kushusha taratibu upendo kwa Carry mwanaume aliyempenda, lakini akawa hapendeki. Kisa ni fukara.”

Baada ya kurudisha kumbukumbu nyuma, alizirejesha tena kwa Carry. Akaufurahia uamuzi wake.

Geti likafunguliwa, haraka haraka, Carry alinyanyuka na kurudi chumbani alipokuwa. Hakutaka mdogo wake kuona jinsi gani anavyojiliza mbele ya James, mwanaume ambaye huko nyuma alimponda na kumdhalilisha.

*************************************

Kama alivyolelewa, James alikuwa na nidhamu, hakumwambia Catty chochote kilichotokea baina yake ya Carry.

Baada ya kula chakula cha usiku ambacho walikuwa wawili tu mezani wakizungumza mambo mengi na kukumbushiana yaliyojitokea huko nyuma, Carry yeye alikula chakula chake chumbani akiwa amejifungia.

Hakutaka kabisa kumuangalia James usoni. Dhamira ilimsuta. Hakukuwa na wa kumsaidia. Si James au Catty.

“Nadhani sasa nikuache Catty. ila nakuahidi nitarudi hapa Jumapili.”

“Eee jamani uje, basi umlete hata huyo wifi yetu tuje kumuona.” James alicheka, halafu akamjibu.

“Nimekwambia ninaye ninayetaka kumuoa. Ila siwezi kuja naye hapa hadi nimuoe.” Catty akaangua kicheko.

James akazama mfukoni, akatoa noti nne za shilingi 10,000 akamkabidhi Catty.

“Hizi ni za maandalizi ya chakula Jumapili, najua wewe ni mtaalam wa kupika, nipikie chakula kizuri kama aulichokuwa unanipikia kipindi kile nilipokuwa naumwa.” Wote waliangua kicheko na kugoneana mikono.

“Na wewe husahau tu!”

“Kwa mapishi yale. Wali samaki mbichi, bamia, nyanya chungu, sijui na nini, weee.”

James alisababisha Catty kucheka hadi machozi yakamtoka. Baada ya kutulia, James akiwa ametulia, akamwambia Catty.

“Nikija Jumapili nakuahidi kwa yote uliuwahi kunifanyia, nikakuletea zawadi kubwa ambayo hutoweza kuisahau.”

“Waooo!!! Haki ya Mungu wala sitolala usingizi, naisubiri hiyo zawadi inafananaje.”

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# KASHTUKA MAPEMA

WASWAHILI wanasema palipo udhia mwaga rupia, ndivyo msanii wa muziki wa R&B, Casandra Ventura, maarufu kama Cassie alivyotumia kwa mpenzi wake wa zamani na rapa mkongwe Sean Diddy Combs ili kupata anachotaka.

Unaambiwa Cessie alikuwa akifanya kazi na Diddy, kisha wakaingia katika mapenzi mazito lakini hali haikuwa shwari muda wote na kujikuta anaishi kama mtumwa wa mapenzi.

Baada ya kuachana muda mrefu, misuguano kati yao ilikuwa ikitawala na ndipo mrembo huyo alipomwaga siri hadharani na kufungua mashtaka kwamba Diddy alimbaka na kumtumikisha katika biashara ya ngono wakati wakiwa wapenzi.

Alisema vitendo hivyo vilimuathiri kisaikolojia na kupelekea kurudi nyuma katika majukumu yake ya kimuziki.

Diddy baada ya kuona Cessie hatanii haraka aliamua kuinua mikono juu na kutaka kumalizana kabla mambo hayajakuwa makubwa.

Taarifa ya pamoja ya wawili hao imesema walifikia makubaliano ya kusuluhisha suala hilo kwa amani siku ya Ijumaa, bila kutoa maelezo ya kina.

Cessie alifungua mashtaka Novemba 16, 2023, akidai Diddy alimpiga, kumbaka, kumuingiza katika matumizi ya vileo, dawa za kulevya na biashara ya ngono kwa zaidi ya Miaka 10.





# Meek Mill afikiria kuacha bangi

Rapa wa Marekani Meek Mill amesema amepanga kuhamia jiji la Dubai, katika Falme za Kiarabu, kwa nia ya kuacha kuvuta bangi.

Meek Mill amesema aligundulika kuwa na matatizo ya emphysema, na alishauriwa na daktari wake kuacha kuvuta sigara na bangi ili kuepuka kukatisha maisha yake.

Kwenye ukurasa wake wa X, Mill aliandika, "Ninaenda Dubai na kuacha kabisa kuvuta sigara. Namfuata Snoop, daktari wangu alisema nilipata ugonjwa wa emphysema ikiwa sitaacha kuvuta sigara nitapunguza nusu ya maisha yangu."

Ameongeza "Nilikuwa mraibu wa nikotini na bangi ililikuwa na kemikali nyingi na hatari sana kucheza na akili yangu!"

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**PARTEY ATAKIWA JUVE**
KLABU ya Juventus imefanya mazungumzo na kiungo wa kati wa Arsenal na Ghana, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 30, kuhusu uwezekano wa kumnunua. (***Foot Mercato***)

**SPURS YAACHANA NA TONEY**
KLABU ya Tottenham Hotspur imeachana na nia yao ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27 ili kujikita katika mipango ya kutaka kumnunua winga wa Barcelona na Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 26 katika dirisha la usajili la Januari. (***Football Transfers***)

**TONEY ANA DENI**
IVAN Toney anahisi kuwa ana "deni la kulipa" kwa Brentford na kuondoka katika klabu hiyo Januari ni jambo linalo mtatiza licha ya Arsenal na Chelsea kuonyesha nia ya kumtaka pia. (***Sun***)

**NEVES AWINDWA**
KLABU ya Newcastle United iko tayari kumsajili kiungo wa kati wa Al-Hilal na Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 26 kwa mkataba wa kudumu Januari iwapo watazuiwa kumpata kwa mkopo. (***90min***)

**MOURINHO ATAKA WALINZI**
KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anataka kuivamia moja ya klabu zake za zamani, Chelsea na kuwasjili mabeki Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 24 raia wa England na Malang Sarr mwenye umri wa miaka 24 raia wa Ufaransa. (***Calciomercato, via Metro***)

**DROGUSIN AWINDWA**
KLABU za Arsenal, Tottenham Hotspur na Newcastle United zinavutiwa na mlinzi wa Genoa na Romania mwenye miaka 21 ambaye thamani yake ni pauni milioni 26, Radu Dragusin. (***Tuttomercato***)

**FATI ANATAKA KUREJEA**
MSHAMBULIAJI wa Hispania, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 21 anataka kurejea Barcelona licha ya kiwango chake kizuri cha uchezaji anachokionesha kwa sasa akiwa kwa mkopo katika klabu ya Brighton. (***Sport***)

**MKATABA MPYA KWA ANCELOTTI**
KLABU ya Real Madrid inatarajia kuongeza mkataba wa kocha, Carlo Ancelotti katika klabu hiyo, huku mkataba wa sasa wa Muitaliano huyo mwenye umri wa miaka 64 ukikamilika mwishoni mwa msimu huu. (***Relevo***)

**FREEDMAN AMWAGIWA SIFA**
MWENYEKITI wa Crystal Palace, Steve Parish amemwagia sifa kemkem mkurugenzi wa michezo, Dougie Freedman, lakini amesema hakujawa na mazungumzo na Manchester United kuhusu uwezekano wa kuondoka. (***Mail***)

**CONGERTON AWINDWA**
MKUU wa idara ya ajira wa klabu Atalanta, Lee Congerton ni mojawapo ya majina yanayozingatiwa na Sir Jim Ratcliffe kuchukua nafasi ya Mkurugenzi wa michezo Manchester United. (***Mirror***)

**NUSA ATAKIWA FULHAM**
KLABU ya Fulham inapanga kumnunua mshambuliaji kinda wa Club Bruges na Norway Antonio Nusa mwenye umri wa miaka 18 Januari. (***Football Insider***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# MBAPPE AZUNGUMZIA BALLON D'OR YA MESSI

**PARIS,** Ufaransa

Amesisitiza nahodha huyo wa Argentina alistahili kutwaa tuzo hiyo kati ya....

KYLIAN Mbappe amesisitiza kwamba, Lionel Messi alistahili kutwaa tuzo ya Ballon d'Or iliyoongeza rekodi kwa mara ya nane baada ya kushinda Kombe la Dunia msimu wa baridi uliopita nchini Qatar.

**Nahodha huyo wa Argentina alijinyakulia sifa hiyo katika hafla iliyofanyika jijini Paris mwezi uliopita, huku Mbappe na Erling Haaland wa Manchester City wakifuatia nafasi ya pili na tatu.**

Messi alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa mashindano nchini Qatar baada ya kufunga mabao saba akiwa njiani kunyanyua taji hilo, akifunga mabao mawili katika ushindi wa mwisho dhidi ya Ufaransa.

Mbappe alifunga hat-trick katika mechi hiyo na alimaliza akiwa na mabao 41 katika mechi 43 katika mashindano yote akiwa na Paris Saint-Germain msimu uliopita - lakini bado anaamini kuwa mchezaji mwenzake wa zamani wa klabu hiyo, Messi alikuwa anastahili tuzo ya Ballon d'Or.

Akizungumza kabla ya mechi ya kesho ya kufuzu kwa Euro 2024 dhidi ya Gibraltar, nahodha huyo wa Ufaransa alisema: "Messi ilibidi ashinde. Alishinda Kombe la Dunia, ni mmoja wa wachezaji bora zaidi katika historia, kama sio bora kwangu.

"Haaland alikuwa na msimu mzuri, mimi pia, lakini karibu na kushinda Kombe la dunia uzani wake ni mkubwa.

"Usiku wa Desemba 18 nilijua kwamba nilikuwa nimepoteza Kombe la Dunia na Ballon d'Or pia. Leo alistahili."

Mbappe pia alizungumzia mchezaji mwingine ambaye anaweza kuwania tuzo ya Ballon d'Or katika miaka ijayo kuwa ni mchezaji mwenzake katikaklabu ya PSG, Warren Zaire-Emery.

Mchezaji huyo wa PSG mwenye umri wa miaka 17 ni sehemu ya kikosi cha Kocha wa timu ya taifa ya Ufaransa Didier Deschamps, baada ya kufunga mabao mawili na kusaidia mengine matano katika mechi 15 za Ligue 1 na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Mbappe aliongeza: "Anavutia. Amekomaa sana, anacheza kwa utu mwingi, haogopi kuchukua mpira, kuleta timu yake kama viungo wa kisasa.

"Sina ushauri wa kumpa, yeye ni mwanzilishi wa PSG akiwa na miaka 17. Hata kama atafanya makosa, atajifunza haraka sana na peke yake."



# CAMAVINGA AIPA PIGO REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Eduardo Camavinga alipasuka mshipa wa goti alipokuwa kwenye majukumu ya kimataifa na Ufaransa wiki hii, klabu hiyo imethibitisha.

Camavinga mwenye umri wa miaka 21 alikuwa akishiriki katika mazoezi na timu ya taifa siku ya Jumatano alipopata jeraha hilo.

Alirejea Madrid kwa ajili ya vipimo, na alifanyiwa uchunguzi zaidi siku ya Ijumaa ili kubaini ukubwa wa tatizo hilo.

"Kufuatia vipimo vilivyofanywa kwa mchezaji wetu Eduardo Camavinga na huduma ya matibabu ya Real Madrid, imegundulika kuwa amepasua mshipa wa goti lake la kulia," ilisema taarifa ya Real Madrid. "Maendeleo zaidi yanasubiriwa."

Camavinga alijiunga na Madrid akitokea Rennes Agosti 2021 na amekuwa kiungo muhimu wa kikosi cha kwanza.

Ameshiriki katika mechi zote 13 za Real Madrid za LaLiga msimu huu, akianza tisa na nne akitokea benchi.

Kikosi cha Madrid kimekumbwa na mfululizo wa majeruhi katika siku za hivi karibuni, hasa katika safu ya kiungo.

Jude Bellingham kwa sasa hayupo akiwa na tatizo la bega, Aurélien Tchouaméni amevunjika mfupa wa mguu wake, kipa Kepa Arrizabalaga hayupo kutokana na jeraha la paja na fowadi Vinícius Júnior aliumia wakati Brazil ikifungwa na Colombia Ijumaa.

Thibaut Courtois na Éder Militão wote hawakuwepo kwa muda mrefu huku wakitokwa na machozi ya ACL.

# Everton yanyang'anywa pointi 10



**LONDON,** England

KLABU ya Everton imekatwa pointi kumi baada ya kubainika kukiuka Kanuni za Fedha za faida na uendelevu za Ligi Kuu ya England (PSR) kwa msimu unaoisha 2021-2022, ligi hiyo imesema.

Adhabu hiyo ni kubwa zaidi ya kimichezo katika historia ya Ligi Kuu England, EPL, na imeihusisha Everton hadi nafasi ya 19 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi nne.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa muda wa Everton, Colin Chong amesema klabu imeshtushwa na kusikitishwa na uamuzi usio wa uwiano na haki na kwamba inakusudia kukata rufani kupinga uamuzi huo.

"Ukali wa adhabu iliyotolewa sio wa haki wala haulingani na ushahidi uliowasilishwa," amesema Chong

Machi mwaka huu Ligi Kuu England iliipeleka Everton katika Tume Huru lakini haikufichua vipengele vilivyokiukwa na klabu hiyo.

Katika kipindi hicho Everton ilitangaza hasara ya fedha kwa mwaka wa tano mfululizo baada ya kuripoti upungufu wa pauni milioni 44.7 kwa mwaka 2021-22.

Klabu za Ligi Kuu England zinaruhusiwa kupoteza pauni milioni 105 kwa kipindi cha miaka mitatu na Everton ilikiri kukiuka kanuni hizo za fedha kwa kipindi kinachoishia 2021-22.

# Barcelona, América mjini Dallas

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA itamenyana na wababe wa Mexico, Club América katika mechi ya kirafiki kwenye Uwanja wa Cotton Bowl wa Dallas mnamo Desemba 21, klabu hiyo ya LaLiga ilitangaza Ijumaa.

Mchezo huo utakuwa wa mwisho kwa Barcelona kabla ya mapumziko yao ya msimu wa baridi na umepangwa siku moja tu baada ya kupangwa kuwakaribisha Almería katika mchezo wa LaLiga.

Itakuwa ni mara ya pili kwa Barcelona kucheza mechi ya kirafiki wakati wa dirisha la Disemba.


Mnamo Desemba 14, 2021, klabu ilisafiri hadi Saudi Arabia kucheza na Boca Juniors kama kumbukumbu ya kifo kwa Diego Maradona.

Vyanzo viliiambia ESPN mwezi uliopita kwamba mechi ya kirafiki iliyopendekezwa nchini Marekani ilikuwa chini ya tathmini na wafanyakazi wa makocha kwa aidha Desemba 21 au 22.

Kocha Xavi Hernandez alikubalika na tarehe hizo kwa kuwa anafahamu hitaji la klabu kuleta mapato, vyanzo vilisema.

Mechi hiyo itakuwa ziara ya pili kwa Barcelona katika uwanja huo wa Cotton Bowl wenye uwezo wa kuchukua watu 90,000. Walicheza na Juventus katika mechi ya kirafiki huko msimu wa joto wa 2022.

Barcelona ilisema mapato kutokana na mchezo huo yatatumika kuchangisha fedha kwa ajili ya wahanga wa kimbunga Otis kilichopiga Acapulco mwezi uliopita na kuua takriban watu 48.



HABARI MICHEZO

## Taifa Stars yaanza vizuri

INATOKA UK. 24

oni mwa kipa huyo aliyeidakia timu ya taifa kwa mara ya kwanza baada ya kutoka majeruhi.

Mkwaju wa faulo wa nahodha Samatta uligonga mwamba wa juu dakika ya 36 na kuikosesha Taifa Stars bao.

Samatta ambaye yeye mwenyewe ndiye aliyeangushwa ndani ya eneo la hatari, alipiga faulo hiyo kwa mkwaju wa juu ambao uliwapita vichwani mabeki wa Niger, lakini kwa bahati mbaya ukaenda kugonga mwamba wa juu kulia kwa kipa Mahamadou Tanja ambaye alikuwa amesimama upande wa kushoto akiuangalia mpira huo.

Kwa matokeo hayo, Stars inakwenda hadi nafasi ya pili katika msimamo wa Kundi E ikiwa na pointi tatu na bao moja, huku kinara wa kundi hilo akiwa Zambia ambayo juzi iliifunga Congo Brazaville mabao 4-2 katika mechi iliyochezwa Uwanja wa Levy Mwanawasa, Ndola, Zambia.

Stars inatarajia kurejea nchini leo kwa ndege ya Serikali iliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya kuiwahi mechi ya Jumanne dhidi ya Morocco katika uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Simba yasaka makali bila kocha mkuu

INATOKA UK. 24

wa Simba, kwa upande wake, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi amesema ameanza programu maalum ya kuwaongezea kasi na maarifa wachezaji wake kuweza kutumia vyema kila nafasi watakayoipata kwenye michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Miguel, alisema anawafanyisha wachezaji wake mazoezi ya kufunga mabao ndani ya eneo la hatari kwa pasi mpenyezo zinazopigwa kutoka pembeni .

"Nataka kuona kila mchezaji anatumia nafasi vizuri ya kufunga kila anapopata nafasi ya kufanya hivyo, kwenye mashindano haya hatupaswi kuwa tunapoteza nafasi yingi za kufunga kama ilivyo sasa," alisema Gamondi na kuongeza,

"Tunajaribu kila mbinu, kila mfumo kwa sababu tunakwenda kucheza mechi ngumu. Tumezoeleka mabao yetu mengi yanapatikana kupitia pembeni, hivyo natengeneza mifumo mingine ambayo tunaweza kubadili pale mmoja unaposhindikana," alisema Gamondi.

Yanga inajiandaa na mchezo wake wa kwanza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria utakaochezwa Novemba 24 ugenini.

# SIMBA QUEENS YASHUSHA MASHINE NYINGINE USAJILI

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumsajili winga kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Isabelle Diakiese, timu ya soka ya wanawake ya Simba Queens imefanya usajili wa mchezaji mwingine Riticia Nabbosa raia wa Uganda kutoka katika klabu ya Fountain Gate Princess.


Kocha wa timu hiyo, Mussa Hassan 'Mgosi' amesema usajili wanaoufanya sasa ni kwa ajili ya kurejesha makali ambayo timu hiyo ilikuwa nayo misimu miwili iliyopita na kupelekea kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, Ubingwa wa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yanayoandaliwa na baraza la Michezo katika ukanda huo (CECAFA) pamoja na kucheza hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita nchini Morocco.

"Tunasajili kwa ajili ya kuziba zile nafasi ambazo zilionekana kuwa na mapungufu lakini msimu huu tunataka kurejesha heshima yetu kwa sababu tuna malengo makubwa hasa kwenye mechi za kimataifa," alisema Mgosi.

Nabbosa ambaye anayeichezea pia timu ya taifa ya Uganda, na pia kuwahi kuichezea Lady Doves ana muda sana kucheza nafasi ya kiungo mshambuliaji.

"Wachezaji wetu bado wana majonzi kwa kile walichokikosa msimu uliopita, nikiwa na maana Ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, wameonekana kuumia na hawajaridhika na kile kilichotokea, kwa hiyo na wao wanaonekana kuwa na uchungu ambao unawafanya kufanya mazoezi kwa bidii, ukichanganya na hawa wapya ambao tunaendelea kuwaongeza, tutakuwa na kikosi bora na kufanya vizuri," alisema Mgosi.

Kikosi hicho ambacho kwa sasa kiko kambini kwa kiasi cha wiki mbili kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa mashindano, kimetamba kuwa kiko tayari na kimeiva kuwakabili Mabingwa wa Tanzania Bara, JKT Queens na Yanga Princess na Fountain Gate katika mechi za Ngao ya Jamii zinazotarajiwa kuanza Desemba 8, kabla ya Ligi Kuu kuanza Desemba 15 au 16.




Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS), Profesa Appolinary Kamuhabwa (wapili kulia), akikabidhi zawadi kwa mshindi wa kwanza katika mbio za urefu wa kilomita tano, Dk Elisha Osati, aliyeshiriki mbio hizo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA** .

# Timu zilizoshuka Ligi Kuu zachakazwa 'Championship'

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za Ruvu Shooting na Polisi Tanzania ambazo zilishuka daraja msimu uliopita kutoka Ligi Kuu Tanzania Bara, juzi zilikiona cha moto zilipotandikwa mabao 3-0 kila moja katika mechi zao za Ligi ya Champoinship inayondelea kutimua vumbi viwanja mbalimbali nchini.

Ruvu Shooting yenye maskani yake mkoani Pwani, ilikung'utwa mabao 3-0 dhidi ya Stand United katika mchezo uliochezwa uwanja wa Mwadui Complex, Shinyanga katika mechi ya raundi ya 11 ya ligi hiyo.

**Mabao ya washindi yali fungwa na Emmanuel Mtambuka dakika ya nane, Maulid Fadhili aki pachika la pili dakika ya 29, kabla ya Said Zanda kufunga la tatu sekunde chache kabla ya ma pumziko.**

Polisi Tanzania nayo ikiwa ugenini, Uwanja wa Black Rhino, Karatu, Arusha, ilijikuta ikiambulia kipigo cha mabao 3-0 kutoka kwa Mbuni FC.

Mbuni ilipata mabao yake kupitia kwa mshambuliaji wa zamani wa Mwadui FC na KMC, Salim Aiyee aliyepachika mawili, kabla ya beki wa kati wa zamani wa Simba, Paul Bukaba, kuweka la tatu.

Matokeo hayo yanaifanya Polisi Tanzania kubaki nafasi ya sita ikiwa na pointi 17 kwa michezo 11 iliyocheza, huku Ruvu Shooting ikiburuza mkia kwa kuambulia pointi moja tu katika ya mechi 11 iliyocheza ikiwa ndiyo timu pekee ambayo haijashinda mechi yoyote mpaka sasa, ikipoteza michezo 10 na kutoa sare moja.


Kwa ushindi iliuoupata Stand United, imefikisha pointi 15 ikiwa nafasi ya nane, Mbuni ikikwea hadi nafasi ya nne ya msimamo kwa pointi 21 ilizonazo.

Michezo
Jumapili Novemba 19, 2023
Nipashe



UKURASA 22

## Camavinga aipa pigo Real Madrid



Winga wa Taifa Stars, Charles M'Mombwa (katikati) akishangilia na nahodha wa timu hiyo Mbwana Samatta na Simon Msuva bao alilofunga jana kwenye mchezo wa kufuzu fainali za Kombe la Dunia 2026 dhidi ya Niger kwenye uwanja wa Marrakech nchini Morocco. **PICHA: MTANDAO**

# Taifa Stars yaanza vizuri safari Kombe la Dunia

## ●●● Sasa kuikabili Morocco Jumanne katika mchezo wake wa pili kuwania....

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya soka ya taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' jana ilianza vyema kampeni yake ya kusaka tiketi ya kucheza Kombe la Dunia mwaka 2026, kwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Niger katika mchezo uliochezwa kwenye uwanja wa Marrakech nchini Morocco.

Niger walichagua kucheza mchezo huo nchini humo kutokana na viwanja vyao kutokidhi vigezo vya Shirikishola Soka Afrika (CAF).

Bao pekee la Stars lilifungwa dakika ya 56 na winga wa kushoto anayecheza soka la kulipwa katika klabu ya Macarthur FC nchini Australia, Charles M'Mombwa.

Bao hilo lilianzia nyuma kwa Bakari Mwamnyeto ambaye alipiga mpira mrefu uliotua katikati ya wachezaji wa timu mbili na katika kunyang'anyana, nahodha Mbwana Samatta aliudhibiti mpira na kupeleka kwenye wingi ya kulia, ukamkuta mfungaji ambaye aliingia nao kwenye eneo la hatari la Niger na kuachia shuti la mguu wa kushoto lililombabatiza beki wa timu hiyo na kujaa wavuni.

Bao hilo pekee linakuwa la kwanza kwa mchezaji huyo mzaliwa na Kigoma, akichezea kwa mara ya kwanza Taifa Stars.

Baada ya bao hilo, Stars ilionekana kucheza kwa tahadhari na kuulinda ushindi wake wa ugenini ambapo kocha Adel Amrouche alifanya mabadiliko kwa kuwaingiza Kibu Denis, Mourice Abraham na Himid Mao kwa ajili ya kuongeza nguvu eneo la kiungo.

Stars ilitumia sekunde 20 tu baada ya kuanza mpira kufika kwenye lango na Niger kwa kuanza na pasi ndefu kuelekea winga ya kulia kwa Simon Msuva, lakini mpira ukaokolewa na mabeki na kuwa kona ambayo nayo hata hivyo haikuza matunda.

Msuva kwa mara nyingine tena alipiga kichwa kuunganisha kona iliyopigwa na Novatus Dismas, lakini mpira huo uliokolewa na mabeki wa Niger.

Niger ilijibu shambulizi hilo dakika ya tano kwa Rahim Alhassane alipoupata mpira akiwa nje kidogo ya eneo la hatari akapiga shuti lililotoka nje kidogo ya lango, huku kipa Aishi Manula akiwa ameruka kuhakikisha.

Ilikuwa ni dakika ya 10, Stars ilipofanya mashambulizi matatu mfululizo ya hatari na la mwisho baada ya makosa ya mabeki wa Niger katika kuokoa mpira ulimkuta, Sospeter Bajana ambaye aliachia shuti kali lililopaa juu ya lango.

Kairou Amoustapha nusura aipatiea Niger bao dakika ya 26, baada ya mabeki wa Stars kuuchezea mpira na kunyang'anywa na Abdoul Moumouni, ambaye alimpenyezea Kairou aliyekuwa amebaki na Manula, lakini shuti lake lilienda mikon-

INAENDELEA UK. 23

## Simba yasaka makali bila kocha mkuu, Yanga ina mfumo mwingine

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally akipita kwenye matawi mbalimbali nchini kuhamasisha mashabiki kujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumamosi ijayo itakapocheza dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, timu hiyo bado inaendelea kunolewa na Kaimu Kocha Mkuu, Daniel Cadena akisaidiwa na Suleimani Matola na huenda ndiyo watakaoisimamia timu hiyo kwenye mchezo dhidi ya Waivory coast hao.

Jana, Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally alikuwa jijini Arusha na kutembelea matawi yote makubwa na kuhamasishana kwa ajili ya mchezo wao wa Novemba 25.

Ahmed alitembelea matawi ya Simba Duniani, Simba Raha Arusha, Arusha Terminal na Simba Burudani.

"Familia ya wanasimba Arusha tumemaliza kujadili hamasa ya mchezo wetu wa Novemba 25 dhidi ya Asec Mimosas.

Viongozi wa matawi yote Arusha wamenihakikishia kuwa watakuja uwanjani na watahamasisha wengine," alisema Ahmed.

Ahmed kwa sasa anatumia nguvu ya ushawishi wake kwenda moja kwa moja kwa mashabiki na matawi yao makubwa nchini kwa ajili ya kurejesha imani kwa wanachama na mashabiki walioipoteza kwa timu hasa baada ya kupokea kipigo cha mabao 5-1 kutoka kwa Yanga.

Baadhi ya mashabiki wamesema kuwa watakwenda uwanjani kuisapoti timu yao na kusahau yaliyopita, hata hivyo wengine wameonekana kuwa na wasiwasi kutokana na kutokuwa na Kocha Mkuu.

Wakati hayo yakijiri upande

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >